

**MAINOO KUIGHARIMU UNITED**

UKURASA 22

**OFISA** mtendaji mbaroni madai kuua mke, yuko hoi kwa kunywa vidonge, pombe



UKURASA 2

**TRA** yaeleza teknolojia ilivyoongeza mapato 2024

UKURASA 5

**SARAKASI** kung'olewa Naibu Rais bado moto

UKURASA 17


epaper.ippmedia.com

MIAKA 30 Nipashe

Mwanga wa Jamii

www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumamosi Oktoba 19, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581834

www.ippmedia.com

epaper.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US 0745 700 710 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital


**RIPOTI MAALUM**

# Utapeli wa viwanja ulivyoacha maumivu



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi.


**WAATHIRIKA** wasimulia walivyoshawishiwa kupitia matangazo... *Endelea Ukurasa wa 4*



UKURASA WA 5

## MAJALIWA ATAJA UMUHIMU WA NIDA KATIKA MATUMIZI YA MIFUMO KIDIGITI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema kila Mtanzania ambaye hajapata namba za NIDA ajiandikishe kwa sababu ni muhimu kuwa nayo wakati huu wanapotumia mifumo ya kidijitali ambayo...



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhi zawadi maalumu ya Mlango wa Zanzibar kwa mgeni wake, Waziri wa Kilimo wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, Dk. Gholamreza Nouri, baada ya kumaliza mazungumzo yao, Ikulu jijini Zanzibar jana. **Habari Uk. 7. PICHA: IKULU**

# Mageuzi bandari kupaisha Zanzibar kiuchumi

UKURASA 2

UKURASA WA 24

## MECHI YA KISASI, HESHIMA

HATIMAYE siku imefika, watani wa jadi nchini, Simba wanatarajia kuikaribisha Yanga katika Dabi ya Kariakoo itakayochezwa leo kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. Mbali na dabi zote...

## Mahakama yatupilia mbali kesi ya Afande

UKURASA 3

**MICHEZO** **TANZANIA YAFUZU AFCON U-20** UK. 23

**KATUNI** UK. 6

# Mfumo ukusanyaji taka kidigitali waja

**Na Mwandishi Wetu**

OFISI ya Makamu wa Rais iko katika mpango wa kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa taarifa za taka ngumu na taka hatarishi katika Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Mfumo huo utasaidia kukusanya taarifa kwa ufanisi, kuchakata maombi ya vibali na kutoa taswira halisi itakayosaidia kufanya maamuzi sahihi kuhusiana na usimamizi wa taka zinazozalishwa.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, alisema hayo jana alipowasilisha taarifa ya hatua iliyofikiwa katika uanzishaji wa mfumo huo wakati wa kikao na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira jijini Dodoma.

Alisema mfumo huu utasaidia kubaini sifa, uwezo na vifaa vya kukusanyia na kusafirisha taka vinavyotumiwa na kampuni zilizopewa kandarasi na halmashauri katika usimamizi wa taka ngumu katika maeneo yao.

Khamis alibainisha kuwa kupitia mfumo huu, serikali itapata taarifa sahihi za hali ya mazingira, changamoto zilizoko na jitihada zake kwa kushirikiana na wadau katika kuboresha mfumo wa usimamizi taka nchini na hivyo kulinda mazingira na afya ya jamii.

"Mfumo huu unatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika kuboresha huduma za usimamizi wa taka ngumu na taka hatarishi nchini. Ni matarajio yetu kuwa, mfumo utasaidia kukuza ufanisi, ufuatiliaji, uwajibikaji na kuimarisha jitihada za uhifadhi, utunzaji na usimamizi wa mazingira," alisema.

Aliongeza kuwa mfumo huo unaoandaliwa chini ya mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira unaotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Maandalizi yake yamefikia 60 na unatarajiwa kukamilika katika mwaka ujao wa fedha.

Naibu Waziri alitaja hatua zinazofuata ni kuendelea kushirikisha wadau ili kubaini mahitaji mengine yanayohitajika kwenye mfumo ikiwamo Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) ili kuukamilisha na kuuboresha kutokana na maendeleo ya teknolojia.

Mfumo utashirikisha watumiaji kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, NEMC, Ofisi ya Rais Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), halmashauri, makandarasi na wadau wengine wanaohusika na usimamizi, ukusanyaji na usafirishaji wa taka zinazozalishwa. Nayo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kupitia kwa Kaimu Mwenyekiti wake, Mhandisi Stella Manyanya, imeonesha kuridhishwa na uanzishwaji wa mfumo huo.

Mhandisi Manyanya pamoja na wajumbe wengine akiwamo Prof. Sukurani Manya, walisema kuna umuhimu wa kutoa na elimu na kuhamasisha wananchi kutenganisha taka ngumu.




Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Alhaj Dk. Abubakar Zubeiry bin Ali, akijiandikisha kwenye Daftari la Wapigakura la Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, katika mtaa wa Kwamndolwa, Kata ya Kwamndolwa, wilayani Korogwe, mkoani Tanga jana. **PICHA: HISANI YA MUHIDINI MICHUZI**

# Mageuzi bandari kupaisha Zanzibar kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema mapinduzi makubwa katika miundombinu ya bandari yanalenga kuifanya Zanzibar kuwa kituo muhimu cha usafirishaji na kupokea meli kubwa zinazoingiza bidhaa nchini.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Mawasiliano, Ikulu, Zanzibar, ilisema Rais Mwinyi alisema hayo jana alipoifungua bandari kavu ya Maruhubi, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema ufunguzi wa bandari kavu ni hatua muhimu ya kuimarisha utendaji wa bandari kwa kuwa itapunguza msongamano wa shehena yakiwamo makontena katika Bandari ya Malindi.

Rais Dk. Mwinyi, kwa mujibu wa taarifa hiyo, alisema mabadiliko hayo ya miundombinu ya bandari yataleta msukumo mkubwa wa ukuaji wa uchumi wa Zanzibar na kuwasisitiza wadau kuunga mkono juhudi hizo.

Alisema kampuni ya Africa Global Logistic inayoendesha bandari ya Malindi hivi sasa inaendelea kuleta mabadiliko makubwa ya kiutendaji yanayoongeza ufanisi na kuwapa urahisi wafanyabiashara kutekeleza wajibu wao bila usumbufu na kuokoa muda.

Dk. Mwinyi aliwahakikishia wadau kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) itaendelea kufanya kazi zaidi na sekta binafsi kwa kuwa mbali ya kuwa na mitaji, pia inakuja na utaalamu na teknolojia za kisiasa zinazochochea ufanisi kwenye utendaji.

Taarifa hiyo ilisema Dk. Mwinyi alisisitiza kuwa serikali inaendelea na ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani kwa kuifanya kuwa yenye uwezo wa kuhudumia meli nyingi zaidi zikiwamo kampuni za kimataifa kuleta meli za mafuta kwenye bandari hiyo.

Alisisitiza kuwa bado kuna fursa zaidi za kuongeza kasi ya utoaji wa huduma kwa bandari zote na kuziagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS), Mamlaka ya Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA), Taasisi ya Nguvu za Atomiki na Mkemia Mkuu wa Serikali kuongeza kasi na ufanisi katika utendaji ili kuwarahisishia wafanyabiashara mazingira bora ya ufanyaji wa biashara yatakayopunguza gharama na kumpa unafuu mtumiaji.

Dk. Mwinyi alibainisha kuwa serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, imedhamiria kuendesha huduma za bandari kwa ufanisi zaidi kwa kuzingatia bandari ni lango kuu la uchumi kwa nchi.

Pia alisema serikali kupitia mradi huo utawapunguzia gharama kubwa wafanyabiashara.

Alisema hatua hiyo pia itasaidia harakati za uendeshaji kuwa zenye ufanisi, kuongeza tija na kupunguza gharama za uletaji mizigo (freight price) ndani ya nchi.

Rais Dk. Mwinyi pia aliwahakikishia wafanyabiashara kuwa serikali inaendelea kuwawekea mazingira rafiki hasa kwa ujenzi wa miundombinu.

Alisema serikali inashirikiana na wadau mbalimbali ili kuendeleza sekta ya uchukuzi na kuimarisha jitihada za pamoja za kuleta mafanikio ya kuimarisha miundombinu ya barabara, bandari na viwanja vya ndege Unguja na Pemba ili kuwarahisishia huduma wananchi na wageni wanaoitembelea Zanzibar.

Dk. Mwinyi aliwasihi wafanyabiashara kuendesha shughuli zao kwa kuwazingatia wananchi hasa kuwapunguzia makali ya bei za bidhaa kutokana na hatua zinazochukuliwa na serikali za kupunguza gharama za usafiri.

Waziri wa Mawasiliano, Usafirishaji na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Muhammed amesema, mageuzi na mafanikio yaliyofikiwa kuimarisha bandari ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025.

Alisisitiza kuwa mabadiliko yanayoendelea kwa kuziimarisha bandari, yataifanya Zanzibar kufikia malengo na matarajio ya kuhudumia meli takriban laki tatu kwa mwaka.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari Zanzibar, Atif Khamis, alisema dhana ya ushirikiano baina ya serikali na sekta binafsi imechochea mabadiliko makubwa ya utendaji wa bandari.

Alisema ufunguzi wa bandari kavu utaongeza mapato ya shirika na kupunguza msongamano wa makontena katika Bandari ya Malindi.

Atif alisema kumekuwa na ongezeko la mapato kwa asilimia 15 tangu kampuni binafsi kuingia ushirikiano na serikali kuiendesha Bandari ya Malindi, kupungua kwa muda wa meli kusubiri gati kwa asilimia 75 na muda wa kutoa makontena kutoka siku 40 hadi siku saba hadi 10 hivi sasa kwa asilimia 50.

# Ofisa Mtendaji mbaroni madai kumuua mke, hoi kwa kuywa sumu

**Na Grace Mwakalinga**

OFISA Mtendaji wa Serikali za Mitaa, Gongo la Mboto, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Dominic Mushi, yuko chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi, akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Amana baada ya kujaribu kujiua kwa kumeza vidonge mbalimbali akiwa amechanganya na pombe aina ya K-Vant.

Mushi alifanya jaribio la kujiua baada kudaiwa kumuua mke wake Dayana Hugo (38) katika nyumba wanayoishi.

Kaimu Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Foka Dinya, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, lilitokea Jumatatu ya wiki hii na kusema mtuhumiwa yuko chini ya ulinzi wa Polisi akipatiwa matibabu baada ya kunywa sumu. Alisema walifika eneo la tukio na kumkuta mtuhumiwa akiwa katika hali mbaya baada ya kumeza vidonge akichanganya na pombe aina ya K-Vant, walilazimika kumkimbiza Hospitali ya Rufani ya Mkoa Amana akiwa chini ya ulinzi.

Kamanda Dinya alisema baada ya mtuhumiwa kupata matibabu na kupona atalazimika kufikishwa mahakamani kujibu tuhuma za mauaji ya mke wake, Diana, aliyekuwa mtumishi wa benki ya NMB.

Akizungumzia tukio hilo, baba wa marehemu, Damian Hugo, alisema walipata wasiwasi baada ya kutomwona binti yao Jumatatu kanisani. Mama yake alipiga na simu ilipokewa na mume wake ambaye aliwaeleza kuwa amefariki dunia. Hugo alisema baada ya kupewa taarifa hiyo, walimtuma pacha wa marehemu aitwaye David ili kufuatilia, alikuta mtuhumiwa akiwa pembeni ya mwili huku akitokwa na povu mdomoni.

"Polisi wanaendelea na uchunguzi wa tukio hilo na mwili wa marehemu unatarajiwa kuzikwa Rombo mkoani Kilimanjaro. Diana ameacha mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi miwili," alisema Hugo.

HABARI KITAIFA

# Mahakama yatupilia mbali malalamiko kesi ya Afande

Na Paul Mabeja, DODOMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Dodoma imetupilia mbali malalamiko yaliyofunguliwa na Wakili Paul Kisabo dhidi ya Fatma Kigondo, maarufu kama Afande, kutokana na dosari mbalimbali zikiwamo kutofuata utaratibu, hivyo kukosa sifa ya kutiwa saini kuwa hati ya mashtaka.

Oktoba 15, mwaka huu, wakili wa mlalamikaji, Peter Madeleka, alimwomba Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Dodoma, Nyambuli Tungaraja, kutia saini malalamiko hayo ili yatumike kama hati ya mashtaka na mshtakiwa asomewe popote alipo ili hatua zingine za kisheria ziendelee.

Akisoma uamuzi wa mahakama hiyo jana kuhusu maombi hayo ya Wakili Madeleka, Hakimu Tungaraja, alisema, mahakama imetupilia mbali malalamiko hayo yaliyofunguliwa na Kisabo dhidi ya Fatma kutokana na kasoro mbalimbali.

Hakimu huyo alisema malalamiko hayo yamekosa sifa ya kuwa hati ya mashtaka kutokana na kutofuata utaratibu wa uandaaji na uwasilishaji.

Alisema moja ya kasoro hizo ni malalamiko kutobainisha kosa la mlalamikiwa wala sehemu lilipofanyika.

"Lakini pia malalamiko haya hayajamtaja mwathirika wa tukio hilo na jina ambalo limetumika la XY halikupaswa kutumika kwa kuwa mwenye mamlaka ya kutoa idhini ya kutumika kwa jina hilo ni mahakama pekee. Mlalamikaji hakuzingatia hilo na kutumia jina hilo kinyume na utaratibu za kimahakama," alisema Tungaraja.

Kadhalika, alisema dosari nyingine ni namna mlalamikaji alivyoandika malalamiko hayo kuwa ni baina ya mlalamikaji na mshtakiwa, jambo ambalo si sahihi.

"Alipaswa kuandika kuwa ni malalamiko baina ya mlalamikaji na mlalamikiwa, lakini yeye ameandika kuwa ni mshtakiwa wakati mtu anakuwa mshtakiwa hadi iwapo hati ya mashtaka, hivyo mahakama hii inatupilia mbali malalamiko hayo na nafasi ya kukataa rufani iko wazi," alisema.

Septemba 5, mwaka huu, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Dodoma, iliahirisha shauri lililofunguliwa na Wakili Kisabo dhidi ya Afande Fatma anayetuhumiwa kuwatuma vijana kumbaka kwa kundi na kumwingilia kinyume na maumbile binti mkazi wa Yombo Dovya, mkoani Dar es Salaam.

Kuahirishwa kwa shauri hilo kulitokana na hakimu aliyekuwa anasikiliza kuhamishwa kituo cha kazi, huku likiwa halijapangiwa hakimu mwingine.

Shauri hilo lilipangwa kusikilizwa Septemba 5, mwaka huu, katika mahakama hiyo na Hakimu Mkazi Fransis Kishenyi.

Kigondo alikuwa anakabiliwa na shtaka la kubaka kwa kundi kinyume na Kifungu cha Sheria Namba 131 A kifungu kidogo cha pili ambacho kinasema, anayewasaidia wahalifu kutenda kosa la ubakaji na yeye anahusika katika ubakaji wa kundi.

Hata hivyo, katika kesi namba 23476 ya mwaka 2024 ya ubakaji kwa kundi na kumwingilia kinyume na maumbile iliyokuwa ikisikilizwa na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Zabibu Mpangule, ilitolewa hukumu yake, Septemba 30, mwaka huu.

Katika hukumu hiyo, washtakiwa wote walikutwa na hatia na kuhukumiwa kifungo cha maisha jela na kulipa Sh. milioni moja kwa kila mmoja na adhabu zote zinakwenda kwa pamoja.

Waliohukumiwa kifungo hicho ni pamoja na askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Clinton Damas, maarufu kama Nyundo, askari Magereza Praygod Mushi, Nickson Jackson maarufu kama Machuche na Amin Lema, maarufu kama Kindamba.

Wote kwa pamoja walikuwa wanakabiliwa na mashtaka ya kubaka kwa kundi na kumwingilia kinyume na maumbile binti huyo aliyetambulishwa kwa jina la XY.



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura akizungumza na Wakuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Wilaya katika kikao kazi, jijini Dodoma jana. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Wawili hufariki kila mwezi Ziwa Victoria

Na Rose Jacob, BUNDA

TAKRIBAN wawili hufariki dunia kila mwezi Bunda mkoani Mara, kutokana na ajali mbalimbali za majini wakati wananchi wakifanya safari na shughuli za kiuchumi ndani ya Ziwa Victoria.

Takwimu hizo zimetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Dk. Vicent Naano, wakati akipokea msaada wa vifaa okozi hususani jaketi 20 kutoka Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria (LVBC) kutokana na ajali ya mtumbwi iliyotokea Septemba 15 katika Kijiji cha Igundu na kusababisha vifo vya watu sita.

Dk. Naano alisema asilimia kubwa ya wakazi wa wilaya hiyo, uchumi wao unategemea Ziwa Victoria na suala la usafiri au shughuli zao ndani ya ziwa ni jambo la kawaida ambalo linakabiliwa na adha ya ajali za mara kwa mara zinazosababisha vifo wilayani humo.

"Tunapokea watu wengi. Kila mwezi lazima kunatokea vifo na tayari tumebaini kuwa vifo vingine vinatokana na watu kutozingatia sheria za usafiri salama majini. Tumeanza kampeni maalum ya kuelimisha jamii kuzingatia suala zima la usalama wawapo majini," alisema Dk. Naano.

Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria, Masinde Bwire, alisema ofisi yake imetoa msaada wa vifaa okozi kutokana na ajali iliyotajwa ya mtumbwi uliokuwa umebeba abiria wakitokea harusini na watu sita kufa maji na wengine 14 kunusurika baada ya mtumbwi huo kuzidiwa na mzigo huku ikidaiwa kuwa haukuwa maalum kwa kusafirisha abiria.

Alisema kuna haja ya mamlaka husika kuchukua hatua za haraka za kudhibiti ajali ambazo zimeendelea kutokea ndani ya ziwa hilo na kusababisha vifo vya watu wengi kila mwaka nchini pamoja na nchi jirani za Kenya na Uganda.

Bwire alisema kamisheni hiyo tayari imeanza kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vituo vya uokozi katika nchi zote tatu, huku kituo kikuu kikijengwa mkoani Mwanza na vitakapokamilika pamoja na mambo mengine vitasaidia kupatikana taarifa kwa haraka za ajali na uokoaji kufanyika mapema.

Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Igundu, wilayani humo, akiwamo Nyanjiga Mafuru, walisema ili kukomesha ajali hizo hatua kali zichukuliwe dhidi ya wamiliki wa mitumbwi ya uvuvi wanaoitumia kusafirisha abiria wakijua leseni zao sio za usafirishaji bali ni za uvuvi.

# Anayedaiwa kumuua mke afariki akipatiwa matibabu

Na Moses Ng'wat, SONGWE

ALLY Mwakilembe (45) anayedaiwa kumuua mke wake, Wema Ndile (32) ambaye walitengana kwa miezi mitano kwa kumchoma visu, amefariki dunia wakati akiendelea na matibabu.

Mwakilembe anadaiwa baada ya kutekeleza mauaji hayo, naye alijichoma kisu tumboni kisha kupelekwa Hospitali ya Wilaya ya Ileje, mkoani Songwe, kwa matibabu na alifariki dunia juzi.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi (ACP) Johnny Maro, katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari, alisema wawili hao ni wakazi wa kijiji cha Kapeta, Kata ya Ikinga, Ileje mkoani Songwe.

Alisema tukio la mauaji hayo lilitokea Jumanne usiku katika kijiji cha Kapeta ambapo Mwakilembe alimshambulia kwa kumchoma visu Ndile sehemu za shingoni na ubavuni upande wa kulia akiwa nyumbani kwake na kusababisha kifo. "Baada ya tukio hilo, Mwakilembe naye alijichoma kisu tumboni na kujisababishia jeraha. Alipelekwa Hospitali ya Wilaya ya Ileje na siku mbili mbele, majira ya saa 9:30 alfajiri, alifariki dunia," alisema.

Alisema wawili hao walikuwa mke na mume ambao walitengana miezi mitano iliyopita na mke alikwenda kuishi sehemu nyingine.

Kamanda Maro alisema uchunguzi wa awali umebaini kuwa chanzo cha tukio hilo ni wivu wa mapenzi.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Maro alitoa wito kwa jamii kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi ili kuepusha kutokea kwa matukio mabaya kama ya mauaji.

Taarifa iliyotolewa awali na Mtendaji wa Kijiji cha Kapeta, Octatus Wangu, ilisema kabla ya mauaji hayo kutokea, mtuhumiwa alikuwa katika harakati za kumshawishi mtalaka wake amrudie baada ya kutengana kwa miezi mitano.

Alisema ndoa ya wawili hao ilidumu kwa kipindi cha miaka 10 na kupata watoto wawili lakini baadaye mwanamke aliamua kutengana na mumewe akimtuhumu kuzidisha ulevi na kusahau majukumu ya familia.

RIPOTI MAALUM

# Utapeli viwanja, mashamba ulivyoacha maumivu

Na Jenifer Gilla

WANANCHI kutoka maeneo mbalimbali nchini wamedai kutapeliwa na kudhulumiwa viwanja na mashamba yao na kampuni inayojihusisha na biashara hiyo ijulikanayo kama Mzalendo Properties yenye ofisi zake Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa wananchi hao, utapeli huo wamefanyika baada ya kusikia matangazo kupitia vyombo vya habari na mitandao.

Mkazi wa Tabata, Dar es Salaam, Suzan Kilamile, akizungumza na mwandishi wa habari hii hivi karibuni, anasema mwaka 2021 alisikia katika chombo kimoja cha habari cha dini (jina limehifadhiwa) tangazo la kampuni hiyo la uuzaji mashamba yaliyoko kijiji cha Buyuni, Vigwaza mkoani Pwani, ndipo akashawishika kuitafuta ili kupata utaratibu.

Anasema aliwasiliana na Ofisa Masoko wa kampuni hiyo aliyemfahamu kwa jina moja la Judy, ambaye alimwelekeza kufika katika ofisi zao zilizoko katika jengo la Millenium Tower, Makumbusho, Dar es Salaam, kwa ajili ya maelezo zaidi.

Kilamile anasema alikwenda katika ofisi hizo na kuelezwa utaratibu ikiwamo kupelekwa katika maeneo ili kuchagua kiwanja au shamba analotaka na kisha kukabidhiwa baada ya kumaliza malipo yote ya Sh. milioni moja.

Anasimulia kuwa Julai, 2021 akiwa na wenzake watano, walipelekwa Buyuni kwa ajili ya kukagua maeneo na baada ya kuridhika alichagua mashamba mawili, moja la kwake na lingine la mdogo wake.

"Sikuwa na wasiwasi wowote kwa sababu baada ya muda tulikwenda tena katika mashamba hayo na kukuta yamepimwa na wakatuonesha ramani," anasema.

Kilamile anasema baada ya kuridhika, mwezi huo alianza malipo ya Sh. 100,000 ya kila mwezi na kumaliza Julai, 2022 kisha akampigia simu ofisa masoko huyo kwa ajili ya kumkabidhi shamba kama mkataba unavyoeleza.

Anasema baada ya hapo usumbufu ulianza na alipowapigia wahusika akiwamo Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, David Mzalendo, alipewa ahadi za kukabidhiwa eneo lake lakini hakuna kilichofanyika.

"Baada ya kuwatafuta kwa njia ya simu miezi mitatu bila mafanikio, nilikwenda katika ofisi zao zilizoko Makumbusho, nikakuta zimefungwa. Mlinzi wa eneo lile aliniambia kuwa walishahama katika jengo hilo na hafahamu waliko," anasema.

Baada ya ahadi za takribani miezi mitatu, anasema alikwenda katika Ofisi ya Kijiji cha Buyuni kujua ukweli wa mambo ndipo Mwenyekiti wa Kijiji hicho, alipomweleza kuwa eneo analozungumzia ni mali ya mtu mwingine.

Anasema mwenyekiti huyo alipomtaka atoe nyaraka ya shamba aliyopewa na kampuni hiyo ili azifanyie kazi, hakuna majibu yoyote hadi sasa.

Mama huyo mwenye wajukuu alioachiwa na mtoto wake aliyefariki dunia miaka sita iliyopita, anasema kinachomuumiza ni kwamba alinunua shamba hilo kwa ajili ya wajukuu zake.

Oktoba 7, mwaka huu, Nipashe ilipomtafuta Mzalendo kwa njia ya simu, alidai kuwa shamba la mama huyo lipo, tatizo ni muda wa kumpeleka eneo husika hajapata.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo alimwomba mwandishi amweleze mama huyo kuwa ampigie simu jioni ili kumsaidia kwa sababu muda huo hana nafasi ya kuzungumza naye.

"Tatizo (la) hao wateja huwa tunawaambia kila siku ukipelekwa katika eneo lako siku ya kwanza shika ramani, maeneo yao yapo ila muda wa kuwapeleka ndio unakosekana, mwambie anitafute jioni nitazungumza naye," anasema.

Ilipofika saa 12: 42 jioni, Kilamile anasema alipompigia simu mkurugenzi huyo, alidai kwamba yuko barabarani, hivyo akitulia atamrudia lakini hakufanya hivyo hadi kesho yake alipomtafuta tena na kujibiwa kuwa, 'nipo msibani, nitakupigia nikitulia.'

Kilamile anasema tangu siku hiyo anapopiga simu hiyo haipokewi, lakini akipiga kwa namba tofauti anapokea na kutoa majibu, hayupo sehemu nzuri atapiga akitulia.

Mkazi wa Mbeya aliyejitambulisha kwa jina Rachel, mwenye mkasa unaofanana na huo, anadai ametapeliwa na kampuni hiyo Sh. milioni 4.3 baada ya kulipia maeneo mawili tofauti yaliyogharimu Sh. milioni 1.7 na Sh. milioni 2.5.

Anasimulia kuwa mwaka 2022 alipelekwa na kampuni hiyo kuona shamba katika Kijiji cha Buyuni na aliporidhika alichukua eneo dogo lenye thamani ya Sh. milioni 1.7 na kulipa deni lote ndani ya miezi sita. alipomaliza alipewa mkataba unaoonesha kuwa amekamilisha malipo, hivyo anastahili kukabidhiwa eneo.

"Nilipokabidhiwa mkataba nikajenga imani na kampuni hii, niongeze eneo lingine lenye thamani ya Sh. milioni 2.2, Ofisa Masoko wa Kampuni hii akanihakikishia kuwa nitapata eneo pembeni ya lile la mwanzo, nililipa fedha zote kwa mara moja," anasimulia.

Anasema akijiandaa kukabidhiwa eneo lake, alipigiwa simu na mwenzake waliyekuwa pamoja siku walipopelekwa kuoneshwa viwanja na kumweleza kuwa inaonekana kuna changamoto katika eneo hilo.

Rachel anasema alipomrejea ofisa masoko kumweleza alichosikia, alimtaka apuuze habari hizo si za kweli.

"Nilifunga safari mpaka katika kiwanja ndipo Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji akaniambia eneo hili ni mali ya mtu mwingine na sisi hatutambui," anasema.

Anasema baada ya taarifa hizo alipomtafuta tena ofisa masoko wa kampuni hiyo, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo na kwamba, wanalishughulikia na baada ya hapo kila akiwatafuta wamekuwa wakimsumbua bila mafanikio.

Joyce Nkya, mkazi wa Sumbawanga, anadai kuwa ametapeliwa Sh. milioni moja kwa utaratibu unaofanana na wenzake, baada ya kulipia eneo alilooneshwa na kampuni hiyo mwaka 2022 wakati huo akiishi Dar es Salaam.

"Niliambiwa kampuni imesajiliwa serikalini. Tangu nianze kudai fedha zangu ni mwaka sasa ninazungushwa, nikipiga simu haipokewi, nikipiga kwa namba nyingine inapokewa na kuzunguzwa.

**MWENYEKITI ASIMULIA**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Vigwaza, Ramadhani Kirumbi, alipotafutwa alisema alipokea wageni katika ofisi yake wakimtaka akawaoneshe maeneo yao waliouziwa na kampuni hiyo, jambo ambalo lilimshangaza kwa kuwa hakuwa na taarifa yoyote.

Alisema alipofuatilia suala hilo aligundua kampuni hiyo iliingia mkataba wa kisheria mahakamani wa kununua eneo lenye ukubwa wa ekari 11 kwa Sh. milioni 80 kutoka kwa mkazi wa kijiji hicho, Amina Mukinda.

Kirumbi alisema kampuni hiyo ililipa Sh. milioni 15 ndani ya muda waliokubaliana na ndipo Amina aliporudi mahakamani na mahakama ikaamua mkataba huo uvunjwe na eneo kurudishiwa kwa mmiliki na hivyo, kampuni hiyo ilipewa eneo lenye ekari mbili kufidia fedha waliokwisha lipa.

Alisema baada ya kugundua ukweli huo, aliwasaidia waliotapeliwa kumtafuta na kumkamata mkurugenzi wa kampuni hiyo na alipokamatwa alithibitisha kuwa alitaka kununua eneo hilo, lakini alishindwa kutimiza makubaliano hivyo si mmiliki wa ardhi hiyo.

"Baada ya kumbana, Mzalendo alitoa lile eneo la hekari mbili na kuwagawia wale waliokuwapo siku aliyokamatwa na eneo lote likaisha. Ninashangaa idadi ya watu wanaokuja kudai maeneo yao bado inaongezeka wakati hakuna lililobaki," alisema.

Alisema kuwa anashindwa kuwasaidia watu hao kwa sababu ofisi yake haina taarifa za mauziano hayo na kuwashauri wanapokwenda kuuziwa maeneo vijijini wahakikishe wanakabidhiwa kwenye ofisi za vijiji ili wajue ukweli wa ardhi inayouzwa.

"Kama watu hawa wangepita katika ofisi yangu wasingefikia hatua ya kutapeliwa, lakini wamepeana juu kwa juu, changamoto hiyo ipo sana, kuna viwanja vinatangazwa kwenye maspika huko kuwa kuna viwanja vinauzwa, lakini sisi wa huku vijijini tunajua wala haviuzwi," alisema.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi

## Bil. 18.5/- kupeleka umeme vijiji 150

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA), umeanza kutekeleza mradi wa kufikisha umeme kwenye vitongoji 150 mkoani Dodoma utakaogharimu bilioni 18.5.

Akizungumza jana kwenye hafla ya kumtambulisha Mkandarasi Derm Group atakayetekeleza mradi huo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alimtaka kuhakikisha anatekeleza kwa viwango na ubora unaotakiwa ili ikamilike kwa wakati na kukidhi matarajio ya serikali.

Alisema upelekaji umeme kwenye vitongoji utasaidia kuchochea maendeleo kwa wananchi wa vitongoji 15 vya kila jimbo la Mkoa wa Dodoma ambao una majimbo 10.

"Kupitia mpango huu tunakwenda kupata vitongoji 150 vipya ambavyo havikuwa na umeme vinakwenda kufikishiwa umeme, mpaka sasa vitongoji vinavyohudumiwa na REA vyenye umeme ni 1,631 na sasa tutakuwa na vitongoji 1,781 vilivyofikiwa na umeme na tunaamini vilivyobaki 1111 vitapata umeme siku zijazo,"alisema.

Alisema kupitia kazi ya REA, Tanzania imeshika nafasi ya pili barani Afrika katika usambazaji wa umeme vijijini.

Naye Mhandisi Msimamizi wa REA Kanda ya Kati, Anneth Malingumu, alisema mradi huo unatarajiwa kunufaisha kaya 4,950.

Alisema kipaumbele cha mradi huo katika maeneo yatakayofikiwa ni huduma za kijamii zikiwamo shule, hospitali, ofisi za serikali za mitaa pamoja na nyumba za ibada.

Alitoa rai kwa wananchi kutunza miundombinu yake ili kuepusha gharama za ziada za matengenezo.

Mwakilishi wa Mkandarasi huyo, Khadija Mukiza, alisema wamejipanga kufanya kazi kwa ufanisi ndani ya muda wa mkataba wa miezi 24.

# TRA yaeleza teknolojia ilivyopaisha ukusanyaji mapato ya robo mwaka

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imetaja sababu ya kuvunja rekodi ya ukusanyaji wa mapato kwa robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha kuwa ni matumizi ya teknolojia za kisasa, hususan Mashine za Kielektroniki za Kodi (EFDs) na Mfumo wa Stempu za Ushuru wa Bidhaa (ETS).

Akizungumza hivi karibuni jijini Dar es Salaam, Kamishna Mkuu wa TRA, Yusufu Mwenda, alisisitiza kuwa mafanikio hayo ni kutokana na usimamizi thabiti wa matumizi ya EFDs na ETS.

TRA ina jukumu la kukusanya Sh. trilioni 29.415 kwa mwaka ikiwa ni sehemu ya bajeti ya kitaifa ya Sh. trilioni 49.3.

Ili kufikia lengo hili, mamlaka ilihitajika kukusanya wastani wa Sh. trilioni 2.45 kwa mwezi.

Hata hivyo, katika miezi mitatu ya kwanza ya mwaka wa fedha, imekusanya Sh. trilioni 7.79, ikiwa na wastani wa Sh. trilioni 2.6 kwa mwezi, na kuvuka malengo ya kila mwezi.

Mwenda alisema mafanikio hayo yameboresha ufuatiliaji wa miamala na ukusanyaji wa ushuru wa bidhaa zinazotozwa kodi.

Alisema mifumo hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa kuhakikisha wanafikia na kuvuka malengo ya mamlaka ya ukusanyaji wa mapato.

Mfumo wa EFDs unafuatilia miamala ya mauzo kwa biashara mbalimbali kuhakikisha kwamba, wanaripoti mapato yao kwa usahihi, hivyo kupunguza ukwepaji wa kodi.

Pia, mfumo wa ETS unafuatilia bidhaa zinazotozwa ushuru kama vile vinywaji, pombe na tumbaku, na kuhakikisha kodi inakusanywa ipasavyo.

Alisema katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha, TRA ilivuka malengo yake, ikifikia asilimia 104 ya lengo mwezi Julai na Agosti, huku mwezi Septemba ikiweka rekodi ya ukusanyaji wa Sh. trilioni 3.18, ambayo ni rekodi mpya ya mwezi mmoja.

Mwenda alisema sera za TRA zinazowatambua walipa kodi kama washirika, zimechangia katika kuboresha mazingira ya utii wa kodi.

Kadhalika alisema TRA imeanzisha mipango kama 'Alhamisi ya Mlipa Kodi,' ambayo inawapa fursa walipa kodi kuwasilisha malalamiko yao na kupata suluhisho kwa wakati.

Alisema TRA imeendelea kushirikiana na wafanyabiashara wakubwa, ambao wamechangia asilimia 43 ya jumla ya mapato yaliyokusanywa katika robo ya kwanza.

Mwenda alisisitiza kuwa utangulizi na utekelezaji mzuri wa teknolojia hizo umechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza ukwepaji wa kodi na kuhakikisha uwazi zaidi katika michakato ya kodi.

"Uboreshaji wa mapato ya Tanzania pia, unakuja sambamba na upaishwaji wa mkataba wa ETS na mtoa huduma SICPA, ambao mfumo wake wa kisasa wa ufuatiliaji wa kodi unasaidia TRA katika kuchukua hatua za utekelezaji," alisema.

Pia alisema sera nzuri zinazowachukulia walipakodi kama washirika, badala ya wapinzani, pia zimechangia mafanikio hayo.

Alisema TRA imeimarisha ushirikiano wake na wafanyabiashara, ikiwa ni pamoja na mipango kama 'Alhamisi ya Mlipakodi,' ambayo inawawezesha walipakodi kutoa malalamiko yao na kupata suluhisho kwa wakati.

"Tumejitoa kusikiliza wafanyabiashara na kuwaunga mkono ili waweze kufanikiwa. Hii, kwa upande mwingine, husaidia kupanua wigo wa walipa kodi," alisema.

Aliwahimiza wafanyabiashara ambao bado hawatii sheria za kodi kujisajili na kuanza kuchangia sehemu yao, hasa wale wanaofanya kazi bila Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN).



Kamishna Mkuu wa TRA, Yusufu Mwenda,

Aliwakumbusha wamiliki wa biashara kwamba, usajili wa TIN ni bure na aliwahimiza kuanza kulipa kodi.

"Tunatoa wito kwa wale wanaoendesha biashara ambazo hazijasajiliwa kujiunga na mfumo rasmi wa kodi na kuchangia maendeleo ya taifa," alisisitiza.

Kuhusu mchango kutoka kwa walipa kodi wakubwa, Mwenda alibainisha kuwa wamechangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa robo ya kwanza.

Kamishna wa Walipakodi Wakubwa, Michael Muhoja, alisema takribani asilimia 43 ya jumla ya mapato yaliyokusanywa na TRA yalitoka kwa wafanyabiashara wakubwa.

"Ningependa kutoa shukrani zangu kwa walipakodi wakubwa wote kwa ushirikiano wao.

"Tumefanya kazi kwa karibu kutoka Julai hadi Septemba, na kujitolea kwao kufuata sheria kumekuwa muhimu kwa mafanikio yetu," alisema Muhoja.

# Majaliwa ataja umuhimu wa NIDA katika matumizi ya mifumo kidigiti

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema kila Mtanzania ambaye hajapata namba za NIDA ajiandikishe kwa sababu ni muhimu kuwa nayo wakati huu wanapotumia mifumo ya kidijitali ambayo inasomana na NIDA.

Majaliwa aliyasema hayo juzi wakati akifunga Kongamano la Nane la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) lililofanyika jijini Dar es Salaam.

Kongamano hilo la siku tano ambalo lilihusisha wadau wa TEHAMA wa ndani na nje ya nchi, limeandaliwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kupitia Tume ya TEHAMA.

Majaliwa ambaye alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan alisema, "Kama utafiti unavyoonesha, hadi mwaka 2030, shughuli nyingi zinazofanywa kwa mkono zitaboreshwa na kuwa za kidijitali." Alisema matumizi ya teknolojia hizo yanaweza kuathiri uaminifu pamoja na masuala ya kimaadili yanayozunguka faragha, umiliki na uwazi.

Kwa muktadha huo, alisema serikali na wadau wote hawana budi kuweka mikakati ambayo itaweza kudurufu matumizi chanya ya teknolojia hizo ambazo kutokana na umuhimu wake haziwezi kukwepeka.

Majaliwa aliitaka wizara husika pamoja na wadau wote kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na Mkuu wa Nchi yanayohusu kuunganisha mifumo yote ya TEHAMA. Pia aliiagiza wizara hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati kutekeleza kwa wakati ujenzi wa Chuo cha TEHAMA mkoani Kigoma. "Wizara isimamie na kuhakikisha ujenzi wa Vituo vya Ubunifu (Innovation Hub) katika mikoa iliyokubalika unafanyika kama ilivyopangwa," aliagiza. Pia aliitaka Tume ya TEHAMA ikamilishe mchakato wa kuanzisha kituo cha kutengeneza na kuboresha vifaa vya TEHAMA (ICT Refurbishment and Assembly Centre).

Kadhalika aliitaka tume hiyo kuendelea kuboresha mfumo wa kuwatambua na kuwasajili wataalamu wa TEHAMA nchini.

Alisema serikali katika mwaka 2020 ilizindua mfumo wa N-Card ambao hadi kufikia sasa imefanikiwa kuwaunganisha wananchi wasiopungua milioni nne.

"Mfumo huu umesaidia sana kuokoa upotevu wa fedha katika vivuko vya Magogoni na Kivukoni. "Vilevile, mfumo huo umesaidia kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato kwenye Kituo cha mabasi cha Magufuli na katika viwanja vyetu vya mpira," alisema. Alisema serikali inaendelea kutekeleza wa Mpango mkakati wa miaka mitano 2024/25 - 2029/30 wa anga za juu utakaoiwezesha Tanzania kurusha satelaiti. Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jerry Silaa, alisema serikali imeendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano ambapo kwa mwaka fedha 2023/24, jumla ya urefu wa kilomita 1,592 za mkongo wa taifa zimejengwa na kufika katika wilaya 83. Pia alisema umoja wa watoa huduma za mawasiliano wamejenga jumla ya kilomita 2,595 ambazo zinafanya mkongo wa taifa kuwa na kilomita 13,820.

Silaa alisema wizara imehamisha shughuli zote zinazohusiana na ujenzi wa mkongo wa taifa wa mawasiliano na Kituo cha Kuhifadhia Data (NIDC) kwenda katika Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL).

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA, Dk. Nkundwe Mwasaga, alisema: "Siku ya pili ya kongamano walikuja vijana wa sekondari wa shule za mchepuo wa Kiingereza na Kiswahili wakaonesha uwezo mkubwa katika teknolojia ya roboti. Imewavutia watu wengi wa ndani na nje ya nchi."

Mtendaji Mkuu wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika (AUDA-NEPAD), Nardos Bekele-Thomas, alimpongeza Rais Samia kwa jitihada anazozifanya katika kuhakikisha Tanzania inatumia ukuaji wa sekta ya TEHAMA katika kuchagiza Maendeleo Endelevu nchini.

Katika kongamano hilo Watanzania ni miongoni mwa waliopewa tuzo kupitia mashindano ya vijana wa Afrika walionesha ubunifu zao katika matumizi ya akili mnemba na roboti.

Majaliwa aliwataka wataalamu wa TEHAMA kujadili namna teknolojia hizo zitakavyotumika kufikia mapinduzi ya nne, tano na sita ya viwanda na hatimaye kuondoa mitazamo kinzani iliyoko kwenye jamii.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba na Yanga, mashabiki msiende na matokeo yenu

**LEO** ndio leo, hatumwi mtoto, mashabiki wa soka ndani na nje ya nchi wanatarajia kushuhudia mchezo mkubwa wa soka la Tanzania na Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati pale Simba watakapoikaribisha Yanga.

Mchezo huo utachezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kuanzia saa 11:00 jioni ni wa mzunguko wa kwanza katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kwa miamba hiyo ya soka nchini.

Ni kawaida kuelekea katika mchezo huo kusikia tambo kutoka sehemu mbalimbali kuanzia kwa mashabiki, wachezaji na viongozi wa timu hizo.

Hata hivyo tunawakumbusha, tumekuwa tukishuhudia matukio mbalimbali uwanjani ya baadhi ya mashabiki kuzimia kutokana na kushindwa kuhimili presha ya mchezo au kukutana na matokeo ambayo hawakuyategemea.

Hii inatokea hasa pale mashabiki wanapokwenda na matokeo yao kichwani kwa kuamini timu yao inauwezo mkubwa na kwa vyovyote watapata ushindi katika dabi hiyo.

Tuwakumbushe soka ni mchezo wa ajabu sana, soka ni mchezo ambao pamoja na burudani, unakuwa na matokeo ya kushangaza muda mwingine, kile unachokitegemea kinaweza kisitokee ukakutana na kile ulichokitarajia kikawa tofauti.

Soka ni mchezo wa makosa, makosa yatakayofanywa na timu A na timu B inaweza ikayatumia kupata matokeo bora kwa kuondoka na ushindi, ni vizuri mashabiki wajiandae na wasiingie uwanjani na matokeo yao mfukoni.

Historia inaonyesha hakuna mchezo mwepesi zinapokutana timu hizi kubwa, maandalizi yake yanaanzia nje hadi ndani ya uwanja na hushirikisha wadau mbalimbali wa klabu hizo pendwa.

Zinapokutana timu hizi kubwa kila mwanachama au kiongozi huungana na kuelekeza nguvu zao kuzisaidia timu zao kupata ushindi, ni mchezo unaobeba hisia kali za mashabiki.

Kwa vyovyote vile, mashabiki wanatakiwa wasubiri mpaka filimbi ya mwisho ili kufahamu nini timu yake itavuna, itapata ushindi, sare au itapoteza, yote haya yatajulikana baada ya dakika 90 kumalizika.

Tunaamini utakuwa mchezo mzuri na wenye upinzani kutokana na ukweli kila timu kwa sasa ina kikosi kizuri, wachezaji wenye uwezo na mabenchi ya ufundi yaliyokamilika.

Lakini pia Nipashe tunawakumbusha waamuzi wa mchezo huu wanaoongozwa na Ramadhan Kayoko wa Dar es Salaam kusimamia vyema sheria 17 za soka ili kupata burudani nzuri na kutoa nafasi timu itakayocheza vizuri kuondoka na matokeo chanya.

Hatusemi waamuzi hawafuati sheria 17 za soka, hapana, tunakumbusha kutokana na presha kubwa ya mchezo huu na Afrika yote macho yao yatakuwa Benjamin Mkapa kuangalia soka na kujua nani ataibuka na ushindi au watagawana pointi.

Hakuna ubishi mchezo huu wa Dabi ya Kariakoo unabeba taswira yote ya soka letu la Tanzania, kupanda kwa viwango vya Ligi Kuu Bara, mpaka kufikia namba sita Afrika, klabu hizi zinamchango wake mkubwa hasa kile wanachokionyesha katika mashindano ya kimataifa wanayoshiriki ambayo yanaandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).


Kwa mantiki hiyo, waamuzi wasitie doa dabi hii, kuharibu mchezo huu ni sawa na kulichafua soka lote la Tanzania, tunaamini watachezesha kwa haki na kutoa nafasi mashabiki kufurahia burudani.

Tunazitakia kila heri timu zote, tunaamini zimefanya maandalizi ya kutosha na zipo tayari kuwapa furaha mashabiki, wanachama na wadau wa soka barani Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mechi 2 za Stars zilizobakia ni machozi, jasho na damu

Na Adam Fungamwango

**MATUMAINI** ya Watanzania kwa timu yao ya Taifa Stars kwenda nchini Morocco kwa ajili ya fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), yamebaki katika michezo miwili iliyobakia ambayo ni dhidi ya Guinea na Ethiopia.

Matokeo ya ushindi ya michezo hiyo ndiyo yatakayowapa Watanzania furaha kwenda AFCON mwakani kwa mara nyingine tena kitu ambacho wameshaanza kukizoea.

Stars itaanza kampeni hizo Novemba 11, mwaka huu ikiwa ugenini dhidi ya Ethiopia, na mchezo wa mwisho utachezwa Novemba 19, mwaka huu nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam dhidi ya Guinea.

Mpaka sasa ni Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), pekee ambayo imeshakata tiketi ya kucheza fainali hizo kutoka katika Kundi H, huku Stars ikiwania tiketi moja iliyobakia na timu hizo mbili.

Ukiangalia ninadharia na kimahesabu Stars bado ina nafasi nzuri mno ya kwenda fainali hizo kama mshindi wa pili.

Inawezekana kabisa DR Congo wasitumie nguvu nyingi au kuwaita wachezaji wake mahiri wanaocheza nje ya bara la Afrika kwa ajili ya mechi zake mbili zilizobaki kwa sababu wameshavuka.

Pamoja na hayo, bado DR Congo ina ubavu wa kutosha kushinda michezo yake yote dhidi ya Ethiopia na Guinea hata kama itaita kikosi cha aina nyingine.

Ni kwa sababu DR Congo bado ina wachezaji bora zaidi ambao haijawaita na hata ambao hawapati nafasi ya kucheza dakika zote 90 kama kina Fiston Mayele, kama wakipewa nao pia watahitaji kuonyesha walichonacho.

Kwa maana hiyo ushindi wa DR Congo dhidi ya Guinea na Ethiopia utakuwa na manufaa zaidi kwa Stars kwa sababu utazidi kuzipunguzia pointi timu hizo.

Binafsi naona DR Congo wana uwezo mkubwa wa kuzifunga timu hizo bila matatizo yoyote, hivyo kazi inabaki kwa Tanzania kuweza kufanya kazi yake.

Unapoomba wenzako wapoteze mechi ni lazima na wewe uwe na uwezo wa kushinda michezo yako ili malengo yako yatimie.

Kwa siku za karibuni kumekuwa kama na tatizo la Taifa Stars kushindwa kupata ushindi kwenye uwanja wake wa nyumbani.

Tunaweza kupata ushindi dhidi ya Ethiopia ugenini, lakini mechi ya mwisho dhidi ya Guinea inaweza kutupa tabu kwa sababu tunacheza nyumbani.

Kwa maana hiyo mikakati kabambe inahitajika ili Stars kushinda michezo yote miwili iliyobaki ili kufuzu AFCON.

Nikisema hivi sina maana mikakati yoyote nje ya uwanja ambayo ni haramu, la hasha, ni ile ya kuhakikisha timu inashinda kihalali.

Maana yangu ni kuifanya michezo hii iwe maalum, kuanzia kuita wachezaji bora na muhimu kwa ajili ya kuifanya hiyo kazi.

Hatuhitaji wachezaji wachanga au wale wanaokomaa, badala yake wanahitaji wachezaji wazoefu zaidi kwenye michuano hii, waliocheza kwa muda mrefu ambao hawana presha na wanaweza kuifanya kazi hii.

Kwa maana hiyo kuna baadhi ya wachezaji ambao waliachwa huko nyuma ni lazima waitwe, warudishwe kwa ajili ya kazi hii tu ya kuhakikisha timu inashinda michezo miwili iliyobaki.

Baada ya timu kutinga AFCON sasa ndiyo tunarudi kwenye mpango wetu na kuita wachezaji wanaofanya vyema kwenye Ligi Kuu, wanaochipukia, vijana na mengineyo kwa ajili ya mipango ya muda mrefu.

Kwa sasa wanahitajika nyota kama Mbwana Samatta, Simon Msuva, Shomari Kapombe, Aishi Manula, Mzamiru Yassin na wengine wengi wazoefu kimkakati na wale wanaofanya vyema kwenye Ligi Kuu waitwe baada ya kufuzu.

# Rais Mwinyi: Kilimo kitaimarisha ushirikiano kidiplomasia na Iran

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameitaja sekta ya kilimo kuwa eneo muhimu litakaloimarisha ushirikiano wa kidiplomasia baina ya Tanzania na Iran.

Amehimiza ushirikiano huo kwa kuisifu Iran kuwa ni wabobezi katika teknolojia ya kilimo.

Rais Mwinyi aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar, alipozungumza na Waziri wa Kilimo wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran, Dk. Gholamreza Nouri, aliyefika na ujumbe wa wataalamu 15 kutoka sekta mbalimbali za maendeleo za nchi hiyo.

Alisema kilimo ni sekta kubwa ya uchumi wa Tanzania Bara kutokana na kubarikiwa kuwa na eneo kubwa kijiografia.

Hivyo, aliishauri Iran kuimarisha ushirikiano kwa kubadilishana uzoefu, mbinu na teknolojia katika eneo hilo.

Kuhusu Zanzibar, Rais Mwinyi alisema, inajikita zaidi katika kilimo cha viungo kutokana na sehemu kubwa ya uchumi wake, kutegemea soko la utalii ambao unachangia asilimia kubwa ya uchumi wa nchi.

Alimweleza mgeni wake huyo kuhusu kuzihuisha na kuziimarisha sehemu za historia katika kukuza soko la utalii wa urithi na kuboresha ushirikiano uliopo baina ya Tanzania hasa Zanzibar na Iran katika eneo hilo la utalii. Pia, aligusia sekta ya usafirishaji wa baharini na kuiomba Iran kuongeza ushirikiano katika eneo hilo, ili kuimarisha biashara na uchumi kupitia bandari za pande mbili hizo za ushirikiano.

Akizungumzia ushirikiano na sekta binafsi baina ya Tanzania hususan Zanzibar na Iran, Rais Mwinyi alimwahidi Waziri huyo kwamba, chemba ya biashara Zanzibar itaimarisha ushirikiano na ya Iran kuona uchumi endelevu baina ya pande mbili hizo.

Waziri Dk. Gholamreza alisifu ushirikiano mzuri wa diplomasia ulioko baina ya nchi hizo mbili na kuongeza kuwa katika kuuboresha wameikaribisha Tanzania nchini kwao na kuwaahidi kuwapa eneo la kufungua Ubalozi wa Tanzania nchini humo.

Pia, waziri huyo alisema watasaini makubaliano na Tanzania hasa Zanzibar katika sekta mbalimbali za maendeleo ikiwamo kilimo, utalii, elimu, biashara na sekta ya uhandisi pamoja na kuahidi kutoa ushirikiano na kubadilishana uzoefu, mbinu na teknolojia kwenye maeneo hayo.

# LATRA yaeleza umuhimu wa e-tiketi ukusanyaji mapato

**Na Grace Mwakalinga**

MAMLAKA ya Usafiri wa Ardhini (LATRA) imeeleza umuhimu wa uwekezaji katika teknolojia ya e-tiketi ili kuboresha ufanisi, uwazi na ukusanyaji wa mapato katika sekta ya usafiri wa umma nchini.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Umma LATRA, Salum Pazzy, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika hafla ya uzinduzi wa filamu ya Daladala Experience iliyofanyika, jijini Dar es Salaam.

Pazzy alisema bado kuna changamoto kubwa katika kuingiza mifumo ya kidijitali katika usafiri wa umma.

"Uwekezaji katika mifumo ya e-tiketi ni hatua muhimu ya kukabiliana na changamoto za usafiri, kwani itasaidia kutatua masuala kama msongamano wa abiria, usalama wa abiria, na ukosefu wa ufanisi katika ukusanyaji wa nauli.

"Mifumo hii itaboresha malipo, kupunguza mizozo ya nauli na kuimarisha usimamizi wa mapato," alisema Pazzy.

Alipongeza ubunifu uliofanyika katika utengenezaji wa filamu hiyo na kusema kuwa, teknolojia iliyotumika inapaswa kuingizwa na taasisi mbalimbali zinazotoa huduma kwa wananchi, ili kuwafikia wengi na kwa wakati.

Mwanzilishi Mwenza na Mkurugenzi wa Taasisi ya Ona Stories, Princely Glorious, alisema kuwa filamu ya Daladala Experience imetumia teknolojia kama vile uhalisia pepe, ikimsaidia mtu kuwa sehemu ya tukio.

"Daladala ni utambulisho wa Mtanzania kutokana na historia yake, licha ya kutengeneza filamu hii, bado tunakaribisha mawazo ya kupata maana halisi ya Mtanzania kwa kuonesha masuala yanayothibitisha uhalisia," alisema.


Glorious alisisitiza kuwa maonesho hayo sio tu yanaangazia urithi wa kitamaduni bali pia, yanatoa jukwaa kwa wasanii kujiweza na kukuza uelewa wa kitamaduni.

Alisema wamewekeza fedha Sh.milioni 104 kuitengeneza filamu hiyo.

Msanii na Mtengenezaji wa Filamu hiyo, Aurelio Mofuga, alisema alishirikiana na wasanii wenzake kutengeneza filamu hiyo ambayo inabeba historia ya nchi na kuwahusisha wazee na vijana.

Mofuga alisema filamu hiyo ambayo ilichukua muda wa miezi sita kukamilika, tayari imeoneshwa katika mataifa mbalimbali, yakiwamo Austria na wanategemea kufanyika maonesho nchini Senegal, Jumatano ijayo.

Mkurugenzi kutoka Taasisi ya Utafiti, Historia, Siasa na Masuala ya Utawala, Said Msonga, alisema serikali inapaswa kuunga mkono jitihada hizo ikiwamo kuboresha mazingira ya utoaji huduma za usafiri wa umma.



Mbeba mizigo akiwa amebeba kiroba cha viazi katika kituo cha daladala cha Mbezi Luis, Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kujipatia ujira wa siku. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wanazuoni kutoa suluhu utekelezaji elimu msingi

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya watafiti 100 kutoka mataifa 10 duniani wamewasilisha machapisho yao yanayolenga kutafuta namna bora elimu ya msingi itakavyotekelezwa.

Hatua hiyo inakuja wakati Tanzania kuna mapitio makubwa katika sera na mitaala ya elimu. Elimu ya msingi inachukuliwa kama nguzo muhimu ya kuandaa watoto kuwa na uwezo na fikra tunduizi, mbunifu na maadili ya Kitanzania.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Wilson Mahera, aliyasema hayo Jumatano wakati akifungua kongamano la siku tatu la elimu lililoandaliwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na kukutanisha watafiti hao ambapo watakuja na mapendekezo ya namna ya kuikuza elimu.

Dk. Mahera aliyemwakilisha Waziri wa wizara hiyo, Prof. Adolf Mkenda, alisema mada zinazowakutanisha watafiti hao ni muhimu na kutaka maarifa yatakayotolewa, yafikishwe wizarani ili kuona namna bora ya kuyatumia katika kuboresha juhudi zinazofanyika.

"Kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, wataalamu hawa watawasilisha machapisho yao na kuweza kujadili namna gani bora elimu msingi inaweza kutekelezwa vizuri," alisema.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Elifas Bisanda, alisema OUT kimekuwa nguzo muhimu katika kuimarisha ubora wa elimu ya msingi nchini.

Alisema chuo hicho kimekuwa kikitoa mafunzo ya stashahada ya elimu ya msingi tangu mwaka 2008, ili kukabiliana na upungufu wa walimu katika ngazi hiyo.

"Pia, kongamano hili ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 30 ya chuo hiki ambacho kimekuwa mbele katika kuendeleza na kuimarisha elimu ya msingi.

"Baada ya kuanzishwa shule za sekondari nyingi kwenye kata, walimu wenye stashahada walihamishwa kufundisha sekondari, hivyo tulianzisha stashahada ya elimu ya msingi na hata walimu waliomaliza, walibaki kufundisha shule hizo wakiwa na maarifa bora zaidi," alisema Prof. Bisanda.

Katibu wa kongamano hilo, Mhadhiri Mwandamizi Dk. Janeth Kigobe, alisema kumekuwa na haja ya kujadili elimu msingi na kuweka mikakati namna ya kushawishi serikali mbalimbali duniani hususani Tanzania, namna ya kukuza elimu msingi kwa manufaa makubwa ya maendeleo ya nchi.

Kabla ya kongamano hilo, kulitanguliwa na matembezi ya hisani yaliyofanyika siku hiyo yakilenga kuhamasisha umma kuhusiana na umuhimu wa elimu msingi nchini.

Washiriki wa kongamano hilo ni wanazuoni kutoka nchi za Uganda, Zambia, Jamaica, Uswisi, Uholanzi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Nigeria, Kenya na wenyeji ni Tanzania Bara na Visiwani.

# Zanzibar yajifunza namna OSHA inavyotekeleza majukumu yake

**Na Frank Monyo**

KAMATI ya Kudumu ya Utalii, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar imetembelea Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) pamoja na baadhi ya viwanda inavyovisimamiwa ili kujifunza na kushauri maboresho stahiki upande wa Zanzibar.

Ziara hiyo imejumuisha wajumbe wa kamati hiyo pamoja na watumishi wa Idara ya Usalama na Afya Kazini iliyoko ndani ya Ofisi ya Rais-Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Zanzibar.

Ukiwa ofisi za OSHA, Dar es Salaam, Mtendaji Mkuu, Khadija Mwenda, kupitia wasilisho lake, alionesha utendaji kazi wa taasisi hiyo, ikiwa ni pamoja na hatua ambazo imepitia kutoka kuwa Idara ya Ukaguzi wa Viwanda katika wizara yenye dhamana ya masuala ya kazi hadi kuwa taasisi inayojitegemea.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mtumwa Peya Yusuph, alisema wanatambua kwamba, OSHA ya Tanzania Bara ipo mbali katika usimamizi wa masuala husika, jambo ambalo limewasukuma kujifunza kwao.

Alisema lengo la ziara hiyo ni ili kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuboresha mfumo wa usimamizi wa masuala ya usalama na afya.

"Tunatambua kwamba wenzetu Bara mnafanya vizuri sana katika usimamizi wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi, hivyo tumeona ni busara kuja kuchukua mazuri yaliyoko ili tushauri serikali yetu kuyafanyia kazi. "Tunawapongeza sana OSHA kwa kazi kubwa wanayofanya katika kuboresha usalama na afya mahali pa kazi, kama tulivyoona katika wasilisho la Mtendaji Mkuu pamoja na hali halisi ya utekelezaji wa miongozo ya OSHA katika viwanda tulivyotembelea," alisema.

Mwenda alisema ziara hiyo ni muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya biashara na uwekezaji Tanzania Bara na Visiwani, kutokana na uhalisia kwamba, wawekezaji wengi wamewekeza kote, hivyo ni muhimu kuwa na mifumo na sheria zinazoendana.

"Tumetia saini hati ya mashirikiano na wenzetu wa Idara ya Usalama na Afya Kazini Zanzibar, hivyo tupo tayari kushirikiana nao katika kufanya maboresho wanayokusudia ili tuwe na mifumo na viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa," alisema Mwenda.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Usalama na Afya Kazini Zanzibar, Ame Faki Saleh, alisema ushirikiano huo utawezesha kufanikisha safari ya mabadiliko ya idara yao kuwa taasisi inayojitegemea kwa upande wa Zanzibar.

Mkurugenzi wa Uhusiano wa Kampuni ya Bakhresa, ambako ni miongoni mwa maeneo yaliyotembelewa na Kamati, Hussein Sufiani, alishuhudia kwamba, kampuni hiyo zimepata mafanikio makubwa katika biashara za ndani na nje ya mipaka ya Tanzania kutokana na kutekeleza ipasavyo sheria za nchi ikiwamo miongozo ya OSHA kuhusu usalama na afya kazini.




Ofisa Mkuu wa Programu na Uendeshaji kutoka Shirika la Kazi Duniani ( ILO), Laura Greene (kulia), Mkurugenzi Mkuu wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Suzanne Ndomba-Ndoran (wa pili kulia), Mkurugenzi wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi, Dk. Kassim Kapalata (wa pili kushoto) na Ofisa Kazi Mkuu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Jane Sorogo, wakizindua Ripoti ya 'Environment Social Government (ESG)', iliyoandaliwa na ATE kwa kushirikiana na ILO, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Wasisitizwa kutobagua watu wanaowatumikia

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU wa Idara ya Oganaizesheni ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Issa Gavu, ametoa wito kwa viongozi wa serikali waliopewa dhamana ya uongozi kuhakikisha wanawatumikia wananchi wa nyanja zote bila kuwabagua.

Akifungua kongamano la kuliombea taifa lililoandaliwa na Kanisa la Ufunuo lililoko Ubungo, mkoani Dar es Salaam, Gavu aliwahakikishia Watanzania kwamba, wataendelea kumwomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwakumbusha na kuwasimamia viongozi wote wa serikali na kila aliyepewa dhamana kutimiza wajibu wake.

"Dhamana waliyopewa viongozi wetu wa serikali ni ya kuwatumikia Watanzania wote bila kujali dini, rangi, kabila na wala jinsia zao," alisema.

Gavu alisema viongozi wa dini ni watu muhimu kwa sababu huliombea taifa pasipo wengine kufahamu na kuwaomba kuendelea kufanya hivyo ili kupata ustahimilivu wa kitaifa.

"Lakini, katika kila jambo unaloliona duniani wapo viongozi wanaochukua jukumu kwa niaba ya wengine, katika jukumu la kumwomba na kumlilia Mungu, niwaombe viongozi wetu wa kiroho, msichoke endeleeni kuliombea taifa.

"Mungu aliyapokea maombi yenu ni baraka na neema kwa taifa lenu. Na viongozi wa kisiasa na serikali msichoke kutukumbusha pale ambako panaondoka amani, upendo na utulivu kwa sababu endapo hayo yatatoweka, hata shughuli za ibada hazitapata nafasi ya kuwapata watu wa kuabudu kwa utulivu," alisema.

Katika kongamano hilo litakalofanyika kwa siku tano, zaidi ya waumini 3,000 wanakutana kuliombea taifa.

# Waziri ahamasisha vijana kujiandikisha kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa

**Na Mwandishi Wetu,**

KIBAKWE

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amewahimiza wananchi hasa vijana kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kwenye Daftari la Makazi ili kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa.

Simbachawene ambaye ni Mbunge wa Kibakwe, amesema zimebaki siku nne tu kazi hiyo ya uandikishaji kufika ukomo, hivyo ni vyema kutumia muda huo kufika kwenye vituo na kujiandikisha.

Alisema hayo juzi kijijini kwao, Pwaga, Kibakwe mkoani Dodoma baada ya kujiandikisha kwenye daftari hilo. Alisema uchaguzi huo ni muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya vitongoji na mitaa kwa ujumla.

Simbachawene aliwataka wananchi kutofautisha uandikishaji wa daftari la makazi unaoratibiwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na ule wa daftari la kudumu la wapigakura unaoratibiwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ( INEC ) kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka ujao.

"Uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa una orodha yake ya wapigakura na uchaguzi ule wa kuchagua Diwani, Mbunge na Rais na wenyewe una daftari lake," alisisitiza.

Kutokana na hatua hiyo, Simbachawene aliwahamasisha wananchi kushiriki katika uandikishaji kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa, hatashiriki kupiga kura katika uchaguzi huo utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu.

Amesema uchaguzi huo ni muhimu kwa kuwa unawapa fursa wananchi kuchagua viongozi wanaoishi nao kwenye mitaa na hao ndio msingi wa mchakato wa shughuli za maendeleo yanapoanzia.

"Msingi wa maendeleo ni watu. Watu hao wakishirikishwa na wakiwa na viongozi wao waliowachagua, watapiga hatua za kimaendeleo kwani ndiko mawazo na ushirikishwaji wa mipango ya maendeleo inakoanzia," alisisitiza.

Aliwataka wananchi hao wajiandikishe ili Novemba 27 wachague viongozi badala ya kuwa watazamaji na walalamikaji kwa kisingizio kuwa hawakuwachagua viongozi walioko madarakani.

Uandikishaji wa wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa ulianza rasmi nchini kote Oktoba 11 na unatarajia kutamatika keshokutwa huku rai kubwa ikitolewa kwa wananchi kujitokeza kwa wingi katika maeneo yao.



# Tume yabaini upungufu sheria mbalimbali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Kurekebisha Sheria Tanzania, imebaini upungufu mbalimbali kwenye sheria nane zikiwamo za uhujumu uchumi na uhalifu wa kupangwa.

Pia imebaini kukosekana kwa chombo mahsusi cha kusimamia na kuratibu masuala ya ulinzi kwa watoa taarifa na mashahidi, kukinzana kwa kanuni za ulinzi za watoa taarifa na mashahidi na sheria ya kuwalinda.

Akitoa juzi taarifa ya tathmini ya mapitio ya sheria hizo, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji wa Mahakama ya Rufani Winfrida Korosso, alisema wamebaini upungufu kwenye sheria zinazosimamia dhamana, sheria ya tathmini ya utekelezaji wa sheria zinazosimamia haki milki na haki shiriki.

"Pia tumebaini upungufu katika utekelezaji wa sheria ya mwenendo wa mashauri ya jinai, uondoshwaji wa mashauri mahakamani, mapitio ya sheria zinazosimamia adhabu ya viboko, sheria ya tathmini ya utekelezaji wa sheria zinazosimamia usafiri wa majini na sheria zinazosimamia usafiri ardhini, hususani kwa njia ya barabara," alisema.

**"Pia tumebaini upungufu katika utekelezaji wa sheria ya mwenendo wa mashauri ya jinai, uondoshwaji wa mashauri mahakamani, mapitio ya sheria zinazosimamia adhabu ya viboko,**

Akizungumza baada ya kupokea taarifa hiyo, Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema kazi walioifanya tume ni kubwa na inahitaji utafiti wa kina ili kupata maboresho yenye tija na kuzifanya sheria ziendane na wakati.

Alisema anaamini mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa hizo yatakidhi kiu na matarajio ya wananchi na wadau wa haki jinai nchini na kuongeza kuwa tayari serikali imeanza kuandaa muswaada.

Hata hivyo, Prof.Kabudi aliitaka tume hiyo kuhakikisha inajitathmini katika utendaji kazi wao ili kuifanya kuwa taasisi ya kufanya utafiti kama zilivyo taasisi zingine za utafiti.

Alitoa rai kwa taasisi zote na wizara zinazofikiria kufanya marekebisho ya sheria, wazipeleke kwenye Tume hiyo,ili izifanyie utafiti wa kina na kutoa mapendekezo ambayo yatasaidia sheria iwe na tija na kutumika kwa muda mrefu.

Aliahidi taarifa ya sheria hizo itawasilishwa bungeni ili zifanyiwe kazi.

# AG ataka Watanzania kujiandikisha uchaguzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

IKIWA imesalia siku moja kufika mwisho wa uandikishaji wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, amewahimiza Watanzania kutumia haki yao ya kikatiba ya kujiandikisha ili kuchagua viongozi watakaowaongoza kwenye maeneo yao.

Johari alisema hayo jana baada ya kujiandikisha kwenye daftari la wakazi kwa ajili ya kushiriki kupiga kura katika kituo cha Mbuyuni, Kata ya Ipagala jijini hapa.

Alisema ni muhimu Watanzania ikiwamo watumishi katika ofisi yake na mawakili wote kuitumia vizuri fursa hiyo.

"Niwaombe watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mawakili wote nchini kushiriki kujiandikisha kwa ajili ya kupiga kura ili kuchagua viongozi wao wa mitaa na kuitumia vizuri haki yao ya kikatiba," alisema Johari.

Pia alisema watumishi wa ofisi yake pamoja na mawakili nchini wanapaswa kutimiza wajibu wao wa kikatiba ambao ni kujiandikisha kwenye daftari la wakazi kwa ajili ya kupiga kura Novemba 27, mwaka huu.

"Kupiga kura ni haki yao kikatiba lakini pia wanao wajibu wa kikatiba ambao ni kujiandikisha kwa ajili ya kupata haki ya kupiga kura na kuwachagua viongozi wanaowataka kwa ajili ya kuwaongoza kwa kipindi kingine cha miaka mingine mitano," alisisitiza.

Uchaguzi wa serikali unatarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu na Watanzania watapata fursa ya kuchagua viongozi katika nafasi mbalimbali wakiwamo wenyeviti wa vijiji, mitaa na vitongoji kwa ajili ya kuwaongoza katika kipindi cha miaka mitano.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji (wa pili kushoto), akiongoza kikao cha Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) cha kujadili masuala ya Muungano, jijini Dodoma jana. Wengine ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi), Hamza Hassan Juma (wa pili kulia), Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhandisi Cyprian Luhemeja (kushoto) na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Salhina Mwita Ameir. **PICHA: OMR**

# Vijana kuwezeshwa vifaa uchongaji madini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Madini kupitia Mpango wa Uchimbaji Madini wa Kesho yenye matumaini (MBT) imejipanga kuwawezesha vifaa na mashine za uchongaji, ukataji na usafishaji madini ghafi kwa vijana watakaohitimu katika Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC) ili kuwa bidhaa bora zenye thamani ya juu.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini alipokuwa akijibu hoja zilizoibuliwa na wajumbe wa kamati hiyo.

Alisema TGC inatoa mafunzo kupitia vifaa vya kisasa husan katika uongezaji thamani madini ya vito kwa ukataji, uchongaji na usafishaji, hivyo kwa mwaka 2024/25 wizara kupitia TGC chini ya mpango wa MBT itawapatia vifaa na mashine za kisasa kwa wahitimu watakaomaliza masomo ili wajiendeleze baada ya masomo kumalizika.

Pia alisema lengo la wizara ni kuwa na kanzidata inayoonesha maendeleo ya wahitimu katika kuendeleza ujuzi wa kiufundi na ubunifu walioupata na kuutumia katika viwanda vya kuongeza thamani madini nchini.

"Mpango mwingine ni kuwapo kwa madini mengi ya vito yaliyoongezewa thamani katika ubora mzuri wa mwonekano, ukataji, rangi na uzito ambayo yatawekwa katika vituo vya biashara ili kutanua masoko ya ndani ya nchi," alisema.

Naye Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, alisema faida za mpango huo kwa wahitimu wa TGC ni pamoja na kuwapatia fursa za masoko, kupata ujuzi wa kisasa kupitia vifaa, kukuza ujasiriamali na kuchangia maendeleo ya sekta hiyo kwa kuongeza thamani madini kabla ya kusafirisha nje ya nchi.

Awali, akiwasilisha taarifa kuhusu utendaji kazi wa kituo hicho, Kaimu Mkuu wa TGC, Mhandisi Ally Maganga, alisema katika kipindi cha Oktoba 2023 mpaka Septemba, mwaka huu, vipande vya madini ya vito 395 yenye uzito wa karati 335.43 vilikatwa.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Kilumbe Ng'enda, aliipongeza wizara na taasisi zake kwa kuratibu na kusimamia mipango mbalimbali inayopangwa ili kutoa matokeo chanya.





# Ajali 16 barabarani zaripotiwa Septemba

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

AJALI 16 zimeripotiwa kwa mwezi wa Septemba, mwaka huu zanzibarr huku katika wilaya ya Magharibi 'B' imeripotiwa kuwa na ajali nne (4) sawa na asilimia 25 ikilinganishwa na wilaya zingine.

Mtakwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Ahmada Hassan Suleiman, alisema jana wakati akitoa takwimu hizo za ajali kwa mwezi huo, Mazizini, Unguja.

Alisema idadi ya ajali hizo za barabarani zilizotokea kwa mwezi Septemba, 2024 zilikuwa idadi sawa na Agosti, mwaka huu, huku wilaya ya Magharibi B ikiripotiwa kuongoza.

Ahmada alisema idadi ya ajali za barabarani kwa mwaka huu zilikuwa sawa na mwezi wa Septemba kwa mwaka uliopita ambao ulikuwa na ajali 16 na kwamba magharibi B imeripotiwa kuwa na ajali hizo nne 4 kwa mwaka huu na kwa mwaka uliopita, kwa mwezi Septemba, wilaya tatu za mkoa wa Mjini Magharibi ambazo ni Mjini , Magharibi A na B zilikuwa na idadi sawa za ajali nne kila moja. Alisema waathirika 24 wameripotiwa kwa mwezi huo wa Septemba, wakiwamo 21 wanaume huku wilaya za Mjini na Wete Pemba zikiripotiwa kuwa na waathirika wengi (watano) sawa na asilimia 20.8.

Alisema waathirika waliofariki dunia kwa mwezi uliopita wameongezeka kwa asilimia 21.4 na kufikia 17 kutoka waathirika 14 waliofariki dunia Agosti, 2024.

Naye Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Zanzibar, Omar Hamad, alisema licha ya kupungua kwa ajali za barabarani, vifo vimeonekana kuongezeka siku hadi siku, hivyo watumiaji wa barabara wanatakiwa kuwa makini wanapo kuwa barabarani.

Aliesema Jeshi la Polisi linaendelea na kusimamia usalama wa vyombo vya usafiri , watumiaji na watembeao kwa miguu na hasa kwa wiki hii ya nenda kwa usalama.

Ofisa Masoko wa Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), Lulu Mohmed Yussuf, alisema shirika hilo linafanya kazi zake kwa karibu na Jeshi la Polisi hasa katika madai ya bima wakati inapotokea ajali .

Alisema wakati umefika ili kuhakikisha gari kabla ya kupasishwa, linakatiwa bima ili kuondoa changamoto mbalimbali hasa kwa mhisika kudharau kwa makusudi au kutoona umuhimu wa bima .

# Othman awafunda wanasheria wajibu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka mawakili na wanasheria kuacha kuutafsiri uwakili kuwa ni kazi ya biashara pekee bali ni kutumikia umma kwa kuzingatia maadili na maslahi mapana ya jamii na taifa kwa jumla.

Othman aliyasema hayo jana ofisini kwake, Migombani, visiwani Zanzibar alipokutana na ujumbe wa Chama cha Wanasheria Zanzibar na kufanya mazungumzo nao kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu utendaji wa mambo ya kisheria nchini.

Alisema wanasheria ni watu muhimu katika nchi na ni lazima kuzingatia maadili ya taaluma yao sambamba na wajibu na msingi wa kuutumikia umma katika kupata haki kwenye maeneo mbalimbali.

Wataalamu wa chama hicho, walisema wanapaswa kuzingatia maslahi mapana ya umma katika kazi na shughuli mbalimbali za kisheria wanazozifanya kwenye utekelezaji wa majukumu yao kama wanavyofanya wanasheria wa nchi zingine kama vile Kenya ambayo ni mfano bora wa kuigwa.

Alisema kuna haja kubwa ya kutekeleza majukumu yao kwa kutetea haki na maslahi ya jamii hasa katika kufuata mfumo mzuri wa kisheria kwa kuwahudumia wananchi.

Othman hali ilivyo sasa inakuwa kama bahati kwa watu kupata haki zao jambo ambalo linapaswa kuwa tofauti iwapo mawakili na wanasheria hawatalitazama suala la haki za watu kibiashara zaidi kuliko maslahi ya umma.

> **Pia aliwataka wanasheria hao kuelewa mfumo wa sheria uliopo nchini hakuna mtu yeyote aliye juu ya sheria na ni wajibu wao kuhakikisha wanachunga na kulinda maslahi ya wote...**

Pia aliwataka wanasheria hao kuelewa mfumo wa sheria ulioko nchini hakuna mtu yeyote aliye juu ya sheria na ni wajibu wao kuhakikisha wanachunga na kulinda maslahi ya wote kisheria bila watu kudhulumiwa.

Alisema ni masikitiko makubwa kwenye uchaguzi wa mwaka 2020 baadhi ya wanasheria walidaiwa kuhusika katika kuharibu uchaguzi kwa asilimia kubwa na kusababisha maafa makubwa kwa jamii. Alisema baadhi ya wanasheria walidiriki kusema uongo na kufanya uamuzi kinyume cha maadili, sheria na taratibu.

Kuhusu elimu ya uraia. Othman aliwataka mawakili hao kuwasaidia wananchi kwa kujipanga vyema kutoa elimu hasa ya uchaguzi.

Katika kufanya hivyo, alisema hawana budi kuwatayarisha wanachama wao kitaaluma ili kuwasaidia wananchi kuepuka haki kutokutendeka na uchaguzi ulete viongozi wanaoweza kuzingatia hatma kwa kila mwananchi wa Zanzibar.

Makamu wa Rais wa Chama cha Wanasheria Zanzibar aliyeongoza ujumbe huo, Hassan Kijogoo, aliiomba serikali kuwashirikisha ipasavyo wanasheria katika utungaji wa sera na sheria mbalimbali kwa maslahi ya nchi.

Alisema chama hicho ni wadau wakubwa na muhimu wa maendeleo na uchumi wa nchi, hivyo kuna haja kwa serikali kuwatumia wataalamu hao ikiwamo katika uanzishwaji wa majadiliano ya mikataba ya kimataifa sambamba na kushirikishwa katika kesi zinazoihusu serikali kwa ndani na nje inaposhtaki au kushtakiwa.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha (wa pili kulia), akiwa na kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa huo, walipotembelea chanzo cha uzalishaji maji cha Ziwa Victoria, katika Kijiji cha Ihelele, wilayani Misungwi, mkoani Mwanza juzi, kinachosimamiwa na kuendeshwa na Mamlaka ya Maji Kahama-Shinyanga (KASHWASA). **PICHA: MARCO MADUHU**

# Watendaji washauriwa kuweka mifumo bora ya afya na usalama mahali pa kazi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WATENDAJI wa Idara ya Usalama na Afya Kazini Zanzibar wametakiwa kuweka miundombinu na mifumo imara itakayowezesha kuimarisha masuala ya usalama na afya kwa wafanyakazi nchini.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi, Mtumwa Peya Yussuf, wakati wa ziara ya kujifunza kwa wajumbe wa kamati hiyo.

Wajumbe wa kamati hiyo walifanya ziara na kukutana na watendaji wa Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar katika masuala ya usalama na afya sehemu za kazi katika Ofisi za Wakala wa Usalama na Afya Mahali Pa Kazi (OSHA), Kinondoni, mkoani Dar es Salaam.

Mtumwa alisema Zanzibar ni sehemu yenye miradi mbalimbali ya kiuchumi ikiwamo hoteli na viwanda na imekuwa nguzo kubwa ya uzalishaji wa ajira nchini, hivyo ni vyema mifumo hiyo kutumika katika maeneo hayo ili kuimarisha usalama na afya za wafanyakazi.

Alisema usalama wa wafanyakazi na afya ni muhimu katika kutekeleza majukumu yao ni jambo na kupewa kipaumbele katika kuhakikisha mifumo hiyo inatumika nchini.

Aidha, aliwashukuru watendaji wa OSHA kwa mafunzo waliyowapatia yatakayowasaidia kuishauri serikali ya Zanzibar kuboresha uwekezaji wa rasilimali watu katika maeneo ya kazi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema katika kuimarisha nguvu kazi ya taifa ni lazima kuwekeza katika afya imara ili kuleta maendeleo.

Alisema lazima mazingira ya kazi yawe rafiki kwa kila mfanyakazi kwa lengo la kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mwenda alisema kwa sasa OSHA imekuwa ni kivutio kikubwa kwa nchi mbalimbali barani Afrika kuja kujifunza kutokana na umahiri na utendaji mzuri wa majukumu yao.

Pia alisema muda umefika sasa kwa Idara ya Usalama na Afya Kazini Zanzibar kuwa taasisi itakayojisimamia na kuweka mikakati imara itakayowawezesha kuingiza pato kubwa kwa serikali.

Wajumbe wa kamati hiyo waliishauri OSHA kuendelea kuziangalia zaidi sekta isiyo rasmi ili kuhakikisha usalama na afya za wafanyakazi zinazingatiwa na kuwashauri kutoa mafunzo hayo kwa wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.



**CHINO**

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI OKTOBA 19, 2024



# DUNIA ITASIMAMA

## Mahakama ikitaja majina waathiriwa wa P Diddy

SIKU chache zijazo dunia inaweza kusimama endapo juhudi za jopo la wanasheria wanaomtetea rapa maarufu wa Marekani, Sean 'Diddy' Combs, kutaka kuwekwa hadharani majina ya waathiriwa wa unyanyasaji wa kingono unaodaiwa kufanywa na mteja wao.

Mawakili hao wanaonekana wameweka ombi hilo wakati wakiwasilisha utayari wao wa kuanza kwa kesi hiyo.

Endapo mahakama itakubali kutaja majina ya waathirika ambao wamejumuishwa katika kesi hiyo, ni wazi dunia itasimama kwa muda kutokana na kutoamini kusikia majina mazito kuhusika.

Hata hivyo, mawakili wa kijana mdogo ambaye aliwasilisha hati mpya za kisheria zilizopatikana na Us, wamejitokeza wakipinga ombi hilo wakitaja ni la kibaguzi na lenye kuchukiza.

Wamesisitiza majina ya waathirika yabaki kuwa siri kwa ajili ya kulinda utu wao.

P Diddy bado anaandamwa na kesi mpya ambazo zinadai mwanamuziki huyo aliwafanyia vitendo vya unyanyasaji wakati waliposhiriki pati yake inayoitwa White Parties'.


Katika hati hizo za maombi zilisomeka kwa kurejea kesi zilizowasilishwa na wanawake wawili na wanaume wanne ambao hawajulikani katika mahakama ya shirikisho ya Manhattan kuweka wazi majina yao.

Rapa huyo kwa sasa anazuiliwa katika gereza la Metropolitan Detention Center lililoko Brooklyn, jijini New York, baada ya kukamatwa Septemba 16.

Lakini, mawakili wa Diddy walidai kwamba faili hizo zilikuwa ni majaribio ya wazi ya kupata umaarufu.

## BASI SAWA

# Diva kutaja baba wa mtoto



MTANGAZAJI maarufu wa kipindi cha mahaba na mahusiano, Diva amesema atamtaja mpenzi wake wa sasa ambaye wanatarajia kupata mtoto.

Akizungumza kupitia kipindi chake, Diva amesema kila kitu kitakuwa hadharani hivi karibuni baada ya kumtaja mwanaume huyo ambaye alimwelezea kama mkarimu na mwenye upendo.

"Natarajia kupata mtoto, ukweli kabisa nitamtaja hivi karibuni baba wa mtoto," amesema Diva.

# Chino aachwe ale bata



MWANAMUZIKI wa Amapiano Chino amesema wamepitia wakati mgumu katika sanaa, kwa sasa ni wakati wa kufurahia maisha.

Akizungumza hivi karibuni, msanii huyo amesema mafanikio anayoyapata kwa kipindi hiki ni kutokana na kuwa na wasimamizi wenye weledi na uchu wa kutafuta soko.

"Nawashukuru viongozi wa timu inayonisimamia kwa kunipa mafanikio haya. Ukweli nilipitia kipindi kigumu katika sanaa, sasa ni wakati wangu wa kufurahia maisha, naomba waniache nifurahi," amesema Chino.



# EU WAIPELEKA ZIFF TANZANIA BARA

FILAMU mbalimbali kutoka nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya (EU) zimeteuliwa kushiriki katika Tamasha la Kimataifa la Filamu la Zanzibar (ZIFF) upande wa Tanzania bara.

Akizungumza katika uzinduzi jana, Mkuu wa Ushirikiano wa Ubalozi wa Umoja wa Ulaya nchini, Marc Stalmans, alisema kuanzia Oktoba 18 hadi Novemba 21, wananchi wa mikoa minne ya Tanzania bara watapata fursa ya kuangalia filamu hizo bure.

Taja mikoa hiyo ni ni Dar Es Salaam, Pwani, Iringa, Arusha na Mwanza.

Stalmans, alisema lengo la tamasha hilo ni kuwajengea uwezo waigizaji na waongozaji filamu wa Tanzania kwa kujifunza kutoka kazi za wenzao wa Ulaya.

Aliesema pamoja na kuonyesha filamu, pia kutakuwa na mafunzo mbalimbali ya namna ya kutengeneza filamu na maudhui .

"Tunataka kuona vijana wetu wanatambua tamaduni mbalimbali kupitia filamu, huko wataona jinsi ya kupambana na changamoto, usawa wa jinsia na kutafakari maisha yetu ya kila siku," alisema Stafmans.

Mkurugenzi Mtendaji wa ZIFF, Joseph Mwale, amwaomba wanancho hasa vijana kujitokeza kwa wingi kuangalia filamu hizo katika kumbi zilizoteuliwa katika mikoa hiyo. Alisema kwa mara ya kwanza filamu za ZIFF zinaonyeshwa katika vyuo vikuu kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi kujifunza na kupata taarifa sahihi kuhusu ufadhili wa masomo katika nchi za Ulaya.

## FILAMU

# Igumba: Kijiji cha Wasiojulikana

**Na Adam Fungamwango**

LEO tunaingalia filamu iitwayo 'Igumba'. Imechezwa na wasanii Amri Athumani maarufu kama mzee Majuto, Amiri Simba, Sabrina Francis, Hashim Kambi, Mark Mfungale, Emmanuel Mtega, Shaaban Hassan na wengineo.

Inazungumzia kisa cha waigizaji ambao walilamzimika kuigiza filamu kwenye kijiji hicho baada ya kutokea matatizo, lakini kilichowatokea hakikuwa cha kawaida.

Jacky, na wengine zaidi ya 15, walitoka jijiji Dar es Salaam kwenda Dodoma kuigiza kwa ajili ya kutengeneza filamu kabambe. Lengo lao ifanye vema kwenye soko ili wajipatie kipato.

Wanafika kwenye pori moja mkoani Dodoma, dereva anatoka kwenda kujisaidia, lakini harudi.

Baada ya baadhi ya wasanii kuingia ndani kidogo porini wanarejea na viatu alivyokuwa amevaa, mwenyewe hajapatikana.

Wasanii wanaamua kuingia ndani kidogo ya pori hilo, na kukuta sehemu moja nzuri ambayo wanaweza kuigiza filamu yao kama kule ambako walitarajia kwenda.

Mmoja wa viongozi wa kijiji hicho, Hashim Kambi anapata habari kuwa kimeingiliwa na wageni ambao haijulikani wametoka wapi.

Anawaambia wanakijiji kuwa jambo hilo halipaswi kudharauliwa kwa sababu haijulikani wana nia gani.

Mzee wa kijiji, mzee Konde anawafuata akiwa na walinzi na kuwaambia waondoke mara moja kwa sababu wameingia bila ruhusa, lakini pia wamevunja mila ya desturi za kijiji hicho.

Wasanii hao watatoa hoja zao kuwa wameingia pale kwa bahati mbaya baada ya dereva wao kupotea, hivyo gari halina dereva na wameamua kufanya 'shooting' kwenye kijiji kile kile, pia hawajavunja sheria yoyote.

Kumbe Igumba ni kijiji ambacho tayari kilikuwa kimeshavunja mila na desturi zake, hivyo mikosi ilianza kukiandama.

Himaya nyingine ilianza kukishambulia kijiji hicho. Ikaita vijana wote ili kupigana na kukitetea kijiji hicho.

Wakati huo huo, kitu kisichojuliana kikiwa porini kilianza kuwashambulia na kuwaua watu kwenye kijiji hicho ikiwamo mpaka wale wasanii.

Wapo waliokufa kwa kukutana au kukutwa na watu wanaopigana vita, lakini wapo waliokuwa wanakufa katika mazingira tata kama alivyopotea dereva wao.

Ikawa ni mshikemshike kijijini hapo, wasanii wao ikawa ni kukimbia kila mmoja kuponyesha roho yake. Pamoja na kusaidiana, lakini pia walikuwa akilaumiana na kukubali kupiga kambi hapo.

Mwisho wa siku hata viongozi wa kijiji hicho walikufa katika mazingira ambayo ilionyesha mizimu imekasirika.

Kijana Jacky na mpenzi wake ndiyo waliobaki hai kati ya wale wasanii zaidi ya 15 walioingia kwenye msitu wa kijiji cha Igumba.

Hawakuamini macho yao walipofanikiwa kujitosa mtoni, kuogelea na kuvuka ng'ambo ya pili, wakiwa salama salimini.







# D Voice hataki umarioo

MWANAMUZIKI anayejipatia umaarufu kutoka Wasafi, D Voice, amesema katika suala la mapenzi mwanaume hawezi kuishi katika nyumba ya mwanamke.

D Voice ambaye anatoka kimapenzi na msanii mwenzake, Lulu Diva, amesema katika mila za kiafrika mwanaume haipendezi kwenda kuishi kwa mwanamke ni jambo la aibu.

Amesema ikifikia wakati wa kuishi pamoja, Lulu Diva ndiye atahamia nyumbani kwake, lakini kwa sasa kila mtu anaishi kwake na wanakutana pale wanapohitaji kuwa pamoja.

# HAKUNA JINA FEKI HAPA

**Na Adam Fungamwango**

KARIBU asilimia 70 mpaka 80 ya wasanii wengi wa muziki duniani hujulikana kwa majina yao maarufu ya kisanii na wala si yale halisi.

Wasanii wengi duniani hutumia majina ya kutungwa na mashabiki au kujitunga wenyewe, yakiwa ama yanalingana na kile kitu wanachokifanya, au kifupi cha majina yao.

Lengo ni kufanya majina yao kutamkika vizuri, tofauti na baadhi ya majina halisi ambayo mengine ni marefu ya hayaonekani kuwa na mvuto mbele ya wanaoyasikia.

Kumekuwa na mlolongo wa wasanii wengi kuwa na majina yao maarufu ambayo si yao halisi, kiasi cha majina yao halisi yasijulikane kwa mashabiki.

Hata hivyo, wapo wasanii wachache ambao wao walivyoingia kwenye tasnia ya sanaa hawakutaka kubadilisha majina na pia waliona kuwa ustaa unatengenezwa na msanii mwenyewe pamoja na ngoma zake na wala si jina. Hawa ni baadhi ya wasanii wa bongo fleva maarufu nchini ambao wanatumia majina yao halisi, lakini bado wamekuwa na ushawishi kwa mashabiki kila kona.

### Ali Kiba

Ni msanii staa zaidi nchini Tanzania ambaye anatumia jina lake halisi. Ni nembo ya muziki wa bongo fleva Tanzania aliyeingia kwenye fani hii mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Kiba ameingia kwenye muziki wa bongo fleva kwa bahati tu, kwani ni mchezaji soka mzuri sana na ilikuwa asajiliwa na moja kati ya timu ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hata hivyo pia alikuwa anajishughulisha na muziki wa kizazi kipya na tayari alikuwa amesharekodi ngoma ya 'Cinderella' iliyompa umaarufu na kuamua kuachana na soka, ingawa pia aliwahi kuichezea Coastal Union kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, misimu miwili iliyopita.

### Banana Zorro

Huyu si msanii tu, ila ni mwanamuziki pia. Ana uwezo wa kupiga muziki laivu ukiwa unapigwa vyombo jukwaani, kitu ambacho si wasanii wengi wanakiweza.

Inawezekana kwa sababu baba yake ni mwanamuziki mkongwe na maarufu nchini, Zahir Ally Zorro aliyewahi kupiga bendi mbalimbali, zikiwamo JKT Mafinga maarufu kama 'Kimulimuli', Sambulumaa, Washirika Tanzania Stars na nyingine nyingi.

Banana ambaye kwa sasa ana bendi yake ya muziki, ni mmoja wa wasanii wachache nchini wataotumia majina yao halisi.

### Vanessa Mdee

Anajitambulisha kwa majina yake yote mawili. Na hata mashabiki wake wanamfahamu kwa majina yake yote. Ukimuuliza mtu msanii 'Vanessa'. Atakuuliza tena Vanessa Mdee?

Imedhihirika kuwa licha ya wasanii wengi duniani kuwa na majina yasiyo halisi. Lakini wasanii wa kike ndiyo wanaoongoza kwa majina ya kubuni. Lakini hili siyo kwa msanii huyu. Amekuwa mahiri pia kwenye muziki kiasi cha kujipatia umaarufu mkubwa.

### Aslay Isihaka

Jina lake halisi ni Aslay Isihaka Nassor. Mwanzoni alijiita Dogo Aslay. Jina ambalo pia halikupindisha jina lake halisi. Na hata sasa ameendelea kujitambulisha kwa jina lake.

Mmoja wasanii vijana kabisa ambao wamekuwa mastaa akiwa wa umri mdogo.

### Mrisho Mpoto

Ni mwimbaji, mtunzi na mashairi. Ana aina yake ya staili ya uimbaji wake ambao ni wa kughani mashairi. Amejipatia umaarufu mkubwa kutokana na aina yake hii muziki ambao maneno na ujumbe wake unafikirisha zaidi kuliko kukupa burudani ya kucheza.

Kutokana na aina yake ya muziki, muonekano, mavazi yake, na hata staili yake ya maisha, wala isingekuwa rahisi kwake kutumia jina la kubuni na kuachana na jina lake halisi.

Ni kwa sababu yeye mwenyewe ni muumini na utamaduni wa Mwafrika na maisha asili.

# Bimbo hataki mapenzi na waigizaji



MWIGIZAJI maarufu kutoka Nollywood, Bimbo Akintola, ametoa sababu za kutoka kimapenzi na wasanii wenzake wa kiume.

Katika mahojiano ya hivi karibuni, msanii huyo alifichua kwamba hakuwahi kuwa na mpenzi mwigizaji kwa sababu anawaona kama kaka zake.

"Sijawahi kuwa na mpenzi na mwigizaji yeyote wakati wowote katika tasnia ya filamu, siwapendi ninyi watu. Sijawahi kuvutiwa na mwigizaji hivyo kusema. Nawaona wote ni ndugu zangu," amesema.



## Mr Macaroni hajaona tatizo

MCHEKESHAJI kutoka Nigeria, Mr Macaroni ameitetea filamu yake fupi ambayo imeibua taharuki baada ya wazazi kudai haifai kuangaliwa na watoto.

Katika filamu hiyo ambayo inamwonyesha mmoja wa watoto wa kike akiwa amevalia kanzu ndogo na sketi ndogo, imekuwa maarufu na watu wazima tofauti na maudhui yake kuwa ya kitoto.

Hata hivyo wengi wamelalamikia maudhui yake na kueleza hayafai kuangaliwa na watoto.

Mr Macaron aliwajibu kwamba ni lazima kuwalea vyema watoto kwa njia aliyoonyesha ili kukuza uimara katika maisha yao na hakuna makosa yoyote katika video hiyo.

## Ini kuolewa sio laana

MSANII wa filamu kutoka Nollywood Ini Edo, amesema hafikirii kufunga ndoa kwa sababu anafurahia maisha aliyonayo sasa.

Akitoa ufafanuzi baada ya video kusambaa mitandaoni ikimwonyesha akiwa kwenye harusi, mwigizaji huyo alisema sherehe hiyo ya harusi ilikuwa ya rafiki yake na yeye alikwenda kama mwalikwa.

"Siwezi kuwa kichaa kuhusu ndoa, sina wazimu huo kujiweka kitanzi katika uhusiano. Sina matumaini na sio hoja zangu kwa sasa," amesema Ini.





## Utata kifo cha Payne

KIFO cha mwanamuziki mkongwe nchini Marekani, Liam Payne, kimezidi kuleta utata kufuatia baadhi ya wafuasi wake kuhoji kama tukio la kuanguka kwake kutoka juu ya ghorofa lina dalili ya kupangwa.

Mwanamuziki huyo ambaye alikuwa mmoja wa wasanii wa bendi ya One Direction, alikufa Jumatano ya wiki hii, baada ya kuanguka kutoka juu ya ghorofa ya hoteli iliyoko Costa Rica nchini Argentina.

Kulingana na TMZ, kabla ya tukio hilo, mwimbaji huyo alileta vurugu hotelini hapo, ikiwamo kuivunja laptop yake na kulazimika kupelekwa kwa nguvu ndani ya chumba chake.

## Gomez amkumbuka maskini

STAA wa muziki wa pop wa Marekani, Selena Gomez, ameonyesha jinsi gani anaguswa na maisha ya watu wa hali ya chini, baada ya kumpa mwanaume mmoja asiye na makazi pesa ya chakula.

Kupitia video iliyosambaa mtandaoni inamwonyesha msanii huyo akimpa mwanaume huyo dola 20 sawa na zaidi ya shilingi 40,000 kwa ajili ya kununulia chakula cha mchana.

Mwimbaji huyo wa "Only Murders In The Building" alikutana na mtu huyo wakati akiondoka katika eneo la Nobu Fifty Seven katika Jiji la New York Jumanne usiku aliposimama kupiga picha kadhaa na mashabiki na kusaini vitabu.





# Vijana mataifa 100 wajadili kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Allan Isack,** ARUMERU

ZAIDI ya vijana 300 kutoka mataifa 100 duniani, wamekutana kwa siku tano katika Chuo cha Maendeleo na Ushirikiano wa Kimataifa (MS TCDC), kupitia kambi ya haki ya hali ya hewa, wakijadiliana namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mratibu wa Kambi ya Haki ya Hali ya Hewa, Augustin Maggio, kutoka Argentina alisema hadi sasa kambi hiyo wameifanya kwa miaka mitatu na kwa miaka miwili iliyopita, walifanya katika eneo la Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini.

"Kambi ya uzinduzi ilifanyika katika nchi ya Tunisia, kisha ikafuata huko Lebanon, ambako mwaka jana iliwashirikisha vijana takribani 500," alisema.

Maggio, alisema wana uzoefu wa kufanya kambi hizo, kuendesha warsha na kutoa mafunzo kwa kuwa kumechangiwa waandaaji, wanaharakati na watetezi kutoka maeneo hayo, kwa ajili ya kubadilisha jamii zao.

"Ujumbe pamoja na shuhuda tunazopata kwa vijana hawa kutoka Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, kuhusu ni kwa namna gani kambi hii inaweza kusaidia kwenye maeneo ya jamii zao.

"Na ni kwamba, tumekuwa tayari kwa muda mrefu kuleta jukwaa hili hapa. Tumekuwa tukifanya kazi na washirika wengi wa ndani kutoka Kenya, Tanzania, Afrika Kusini, Uganda na hatimaye tuliweza kuiweka pamoja," alisema.

Pia alisema kambi hiyo imeunganishwa na zaidi ya mashirika 30 ya wanaharakati na watetezi wa haki za binadamu, yakiwamo kutoka nchini na nje ya nchi.

Naye Hapyness Njile kutoka Taasisi ya Agline Peace Africa, alisema jukwaa hilo limewakutanisha vijana kwa kuwa imeonekana wao ndio waathirika wakubwa wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

"Tumekutana hapa kuangalia ni namna gani tutakavyoweza kupambana na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa kundi la vijana wamekuwa wahanga kwa kuwa wana wajibika kwenye sekta zote ikiwamo kilimo na uchimbaji madini," alisema.

Alisema katika jukwaa hilo, amejifunza namna ya kwenda kuelimisha jamii ikiwamo kutunza mazingira hasa kutokukutupa taka ovyo na kukata miti kwa ajili ya shughuli za kibinadamu.

Mdau wa mazingira na mshiriki katika kambi hiyo kutoka Taasisi ya Green Conserver, Ziada Kassim, alisema wamekuwa wakishiriki katika harakati za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, utunzaji wa mazingira pamoja na nishati mbadala.

"Athari za mabadiliko ya tabianchi, inaweza kuchangia kushuka kwa nchi kimaendeleo kwa hiyo kijana anapaswa kuwa mstari wa mbele kupambana na athari hizo kwa kuwa ndio nguvu kazi tuliyonayo kwa sasa," alisema.



Kaimu Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Nyenza Michael, akizungumza na waandishi wa habari kutoka Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), waliofika wilayani humo mkoani Tanga mapema wiki hii, kwa ajili ya ziara ya kimafunzo kupitia mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ruzuku yaongeza matumizi ya mbolea

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

UAMUZI wa serikali wa kutoa mbolea ya ruzuku kwa wakulima nchini, umesaidia kuongeza matumizi ya mbolea kutoka tani 360,000 mwaka 2022 hadi tani 840,000 za sasa, sawa na ongezeko la asilimia 131.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Dk. Mohamed Hussein Omary, akizungumza jana mjini hapa, alisema mbali na kuongezeka kwa matumizi ya mbolea, pia kuna tija ya mahindi imeongezeka kutoka tani 1.9 kwa ekari moja, mpaka tani mbili kwa sasa.

Maharagwe tija yake imeongezeka kutoka kilogramu 800 kwa ekari mpaka kilogramu 1,000 kwa sasa.

Alisema wakati serikali inaanza kutoa ruzuku mwaka 2022, matumizi ya mbolea yalikuwa tani 360,000 na mwaka 2021, matumizi ya mbolea yalikuwa zaidi ya tani 500,000 lakini sasa hivi yako zaidi ya tani milioni 1.2.

Alisema ni vizuri wakulima wakawa na bima za kilimo ili kujikinga na majanga ya ukame, mafuriko na kimbunga, ambapo alitoa mfano wa nchi ya Zambia, ambayo imeomba kupelekewa tani 650,000 baada ya kuwa na ukame. Nchi nyingine zilizoomba, ni Malawi na Congo DRC.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Kudhibiti Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, alisema mwaka 2023/24 walilenga kufanya ukaguzi wafanyabiashara 3,400 ila walikagua 3,737.

Pia alisema msimu wa kilimo wa mwaka 2024/25 watapima mashamba ya wakulima waliosajiliwa kwenye ruzuku na kuwapatia hati miliki ili waweze kuzitumia kukopa kwenye taasisi za fedha.

Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Veronica Kessy, akizungumza katika maonyesho hayo, naye alisema mwaka jana serikali ilitoa ruzuku tani 11,346 kwa wakulima.

Kuhusu maelekezo ya serikali, Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Manyara cha Rift Valley Cooperative Union (RIVACU), Pendael Valentine, alisema walishaanza kuchukua hatua na wamepewa uwakala wa kusambaza mbolea ya Minjingu na Yara kwa wakulima.

Alisema bila kutumia mbolea huwezi kupata mavuno ya kutosha na sasa hivi wao wanahamasisha kupima afya ya udongo kwanza wakulima kwenye mashamba yao.

Meneja huyo, alisisitiza mazao wanayoyapa kipaumbele kuwa ni zao la kahawa, pamba, vitunguu saumu, miwa na dengu.

# Mkenda aipa kongole shule mchango elimu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameipa kongole Shule ya Turkish Maarif Foundation ya Arusha, kwa mchango wao mkubwa katika sekta ya elimu nchini Tanzania.

Aidha, Prof. Mkenda ameishukuru serikali ya Uturuki kwa kuisaidia serikali ya Tanzania kuhakikisha watoto wanapata elimu bora kama inavyotakiwa na kuwa na sera inayosisitiza kila mtoto kupata elimu bora.

Prof. Mkenda aliwakilishwa katika mahafali ya wanafunzi wa darasa la saba na kidato cha nne wa shule hiyo na Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa.

Alipongeza shule hiyo kwa kufanya vizuri kitaaluma sanjari na kutumia mtaala wa nchini katika ufundishaji wake na inaajiri Watanzania katika maeneo ya kufundisha na yasiyo ya kufundisha.

"Nina furaha sana kusikia kwamba shule hii, kwa kushirikiana na SOS Children's Villages, inatoa ufadhili wa asilimia 100 kwa watoto kutoka familia zenye mazingira magumu kwa ajili ya masomo yao kuanzia chekechea hadi ngazi ya juu," alisema Dk. Mtahabwa.

Mkuu wa Sekondari ya Turkish Maarif Foundation Arusha, Kheri Abubakar, alisema shule imekuwa ikifanya vizuri kwenye matokeo ya mtihani wa kitaifa tokea ilipoanza mwaka 2020.

Alisema matokeo ya kidato cha sita ya mwaka 2023/2024, wanafunzi wanne walipata daraja la kwanza watano daraja la pili, wanne daraja la tatu na mmoja daraja la nne.

Pia alisema katika mtihani uliofuata wa mwaka 2024, matokeo yalipanda kwa kiasi kikubwa, ambapo wanafunzi 16 walipata daraja la kwanza, saba wakapata daraja la pili na mmoja daraja la tatu. Akizungumzia matokeo ya mwaka 2023 ya kidato cha nne, Abubakar alisema wanafunzi 12 walipata daraja la kwanza, wanafunzi 13 daraja la pili na wengine saba wakipata daraja la tatu.

Hata hivyo, alisema hali ilibadilika mwaka unaofuata ambapo wanafunzi 21 walipata daraja la kwanza, 18 daraja la pili na wanne daraja la tatu.

Cengiz Polat, Mkurugenzi wa Shule za Maarif za Kituruki Tanzania, alieleza kuwa watoto wanaosoma kwenye shule zao wanapata fursa nyingi ikiwamo ufadhili wa masomo ya elimu ya juu nchini Uturuki kwa asilimia 100.

"Nitawapa habari njema. Hivi sasa tunafanya kazi katika nchi 54, zikiwa na shule 477 zinazofundisha zaidi ya wanafunzi 55,000 duniani. Tunaamini tunafanya athari chanya kwa kuwekeza katika uwezo wa binadamu.

"Wahitimu kutoka shule hii hawataimarisha tu nchi zao bali pia kuimarisha uhusiano kati ya Uturuki na Tanzania," alisema.

Naye Ahmed Sami Demir, Mkurugenzi wa Turkish Maarif Arusha, alieleza kujivunia mafanikio ya wahitimu yanavyoendelea kuboreka mwaka hadi mwaka.

## TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Kifo cha Boyibanda kilivyoongeza huzuni miaka 35 ya Franco kaburini

**Na Adam Fungamwango**



Mwanamuziki, kiongozi wa bendi ya TP OK Jazz, ambaye Oktoba 12 mwaka huu, alifikisha miaka 35 tangu alipofariki dunia 1989 nchini Ubelgiji.

WAKATI mashabiki wa muziki wa rhumba duniani wakiwa wanajiandaa kuadhimisha miaka 35 ya kifo cha gwiji wa muziki huo, Franco Luambo Makiadi, wamejikuta wamepata pigo lingine walipotangaziwa kifo cha Michel Boyibanda, mmoja wa waimbaji mashuhuri wa bendi ya TP Ok Jazz, iliokuwa ikiongozwa na Franco.

Mwanamuziki huyo aliyekuwa na miaka 84, alifariki Jumanne iliyopita katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Brazzaville.

Boyibanda alikuwa miongoni mwa wanachama wachache waliobaki wa TP OK Jazz, na kulingana na ripoti kutoka jiji la Congo Brazaville, alifariki dunia kutokana na matatizo ya kiharusi ambayo yalimpata 2015.

Kifo chake kimeleta simanzi kwa wanamuziki na mashabiki wa muziki wa dansi, hasa rhumba, pamoja na wanamuziki wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Congo Brazaville.

Mwanamuziki na mtayarishaji wa muziki kutoka Kinshasa, Maika Munan, alikiri kuwa Boyibanda mwanamuziki bora kabisa kwani alikuwa na uwezo wa kutunga, kuimba na kucheza.

Alikuwa ni mmoja wa wanamuziki wachache walioweza kutoka Congo Brazaville na kwenda kupiga muziki DR Congo, ambapo wengine waliwahi kufanya hivyo ni ,Jean Serge Essous, Edo Nganga, na Celestin Kouka, ambao walijulikana walipovuka kutoka Brazzaville kwenda Kinshasa kutafuta fursa bora za muziki.

Kabla ya kujiunga na TP OK Jazz mwaka 1964, Boyibanda alikuwa akifanya kazi na Negro Band huko Brazzaville na pia alishiriki katika makundi mengine kama Les Freres, Rumbaya na Cercle Jazz.

Katika mahojiano ya televisheni Kinshasa, mwanamuziki hiyo walisimulia jinsi kila Jumatatu alivyokuwa akijiunga na wanamuziki wengine wa OK Jazz kwenda kumburudisha Rais Mobutu Seseseko wa Zaire wakati huo katika makazi yake rasmi, ikulu.

Uhodari wake wa kuimba na kucheza ndiyo uliofanya awe anachulikuwa kutoka nchini kwao kuungana na bendi ya Franco, baadaye akapata ajira rasmi na kuwa mwananuziki wa bendi hiyo.

Kwa miaka ya karibuni hakuna shabiki yoyote wa muziki aliyesikia wala kujua habari zake, kutokana na matatizo ya afya, lakini mashabiki wake wa muda mrefu wataendelea kukumbuka uhodari wake akiwa jukwaani, hasa umahiri kwenye uchezaji wake hasa kwenye kutikisa mwili na miguu, kiasi cha kuleta burudani.

Alikuwa mmoja wa wanamuziki wachache waimbaji waliokuwa wakiwafanya mashabiki badala ya kucheza kumtazama yeye kutokana na ustadi wake wa kutumia mwili wake katika uchezaji wa muziki licha ya kuwa mwimbaji stadi pia.

Alikuwa akionekana kwenye chaneli maarufu ya muziki wa DR Congo wakati huo, Tele Zaire katika miaka ya 1970, akiimba pamoja na waimbaji wengine nyota kama, Wuta Mayi, Sam Mangwana, Youlou Mabiala na wengineo.

Alikumbukwa kwa nyimbo zake kama "Zando ya Tipo Tipo," "Salima," "Esololaka," na nyinginezo.



Boyibanda



Mwimbaji, mtunzi na mwanamuziki wa zamani wa bendi ya TP OK Jazz, iliyokuwa ikiongozwa na Luambo Luanzo Makiadi, Franco, aliyefariki dunia Jumanne iliyopita nyumbani kwao nchini Congo Brazaville, akiwa na miaka 84.

# SARAKASI TUPU KENYA

## -Uteuzi Naibu Rais mpya wasitishwa
## -Gachagua arudishwa na mahakama



Rigathi Gachagua

**NAIROBI,** KENYA

NI kama mchezo wa sarakasi unaoendelea katika siasa za Kenya, kwa kuwa Mahakama Kuu ya nchi hiyo imesitisha uteuzi wa Naibu Rais mpya, baada ya Bunge la Seneti kupiga kura ya kumwondoa katika wadhifa huo, Rigathi Gachagua.

Naibu rais mpya aliyeteuliwa kushika nafasi hiyo ambayo ilikuwa wazi kutokana na uamuzi huo ni Kithure Kindiki na kuidhinishwa kwa kura nyingi na wabunge.

Mchakato wa kumwondoa Naibu Rais Gachagua, ulikamilika baada ya seneti kupiga kura usiku wa kuamkia jana, na ndipo Rais William Ruto kwa haraka aliwasilisha bungeni jina la Kindiki, kushika nafasi hiyo.

Wabunge 236 walipiga kura ya kukubali uteuzi wa Kindiki kushika nafasi hiyo.

Kilichosubiriwa ni jina lake kuchapishwa katika gazeti rasmi la serikali na kisha kuapishwa kwa ajili ya kuanza majukumu yake hayo mapya kama Naibu Rais .

Hata hivyo, jana alasiri mahakama kuu imesitisha utekelezwaji wa azimio la Seneti la kumwondoa madarakani Rigathi Gachagua.

Mahakama ilitoa uamuzi wa kuamuru Gachagua kuendelea na nafasi yake.

Hapo jana maseneta nchini humo walikubali mashtaka matano kati ya 11 dhidi ya Gachagua na kumpigia kura ya kumwondoa madarakani.

Hata hivyo, Gachagua alishindwa kufika mbele ya kikao cha seneti kujitetea baada ya mawakili wake kueleza kuwa alipatwa na tatizo la maumivu makali ya kifua' na kulazimika kulazwa hospitalini.

Katika uamuzi wa jaji E.C. Mwita, umezuia kutekelezwa kwa azimio hilo la seneti na pia kuzuia rais kumteua mtu kuichukua nafasi hiyo hadi Oktoba 24, kesi hiyo itakapotolewa hukumu na majaji watatu ambao walioteuliwa kuisikiliza na Jaji Mkuu Martha Koome.

Kumekuwa na hali ya kigugumizi kutokana na Rais Ruto kupendekeza jina la Kithure Kindiki kuichukua nafasi ya Gachagua na bunge la taifa pia kuafiki uteuzi wake.

Katiba ya nchi hiyo inasema pindi rais anapowasilisha uteuzi kwenye Bunge, wabunge watapiga kura ya kulikataa au kuiidhinisha jina hilo. Pia hakuna sharti la kura ya theluthi mbili.

Prof. Kindiki, ambaye kwa sasa ni Waziri wa Mambo ya Ndani na Utawala wa Kitaifa, atahitaji idhini ya bunge kabla ya kushika nafasi ya Naibu Rais.

Bunge latalazimika kupiga kura ya uteuzi ndani ya siku 60 baada ya kupokea jina hilo.

Baada ya kuidhinishwa, mteule atateuliwa rasmi na Rais kuwa naibu wake.

Ingawa katiba haijaweka bayana nini kinaweza kutokea ikiwa utasimamishwa na mahakama endapo bunge limeidhinisha.

Katika maandalizi ya uchaguzi mkuu wa 2022, Kindiki alikuwa miongoni mwa watu waliopendekezwa kuwa mgombea mwenza wa Ruto, lakini akaamua kumchagua Gachagua.



Prof.-Kithure-Kindiki

Baadaye Ruto alielezea kwamba alimchagua Gachagua kwa sababu ya umri wake na alifikiri wangeelewana zaidi.

Wakati mchakato wa kumuondoa madarakani Gachaguo, Rais Ruto alikuwa na mazungumzo na Kindiki kukubali kuchukua nafasi yake.

**Profesa Kithure Kindiki**

Abraham Kithure Kindiki alizaliwa Julai 1, 1972 ni mwanasiasa na wakili msomi wa Kenya ambaye kwa sasa ni Waziri wa Mambo ya Ndani na Utawala wa Serikali ya Kitaifa.

Aliwakilisha Kaunti ya Tharaka-Nithi katika Seneti ya Kenya kuanzia 2013 hadi 2022.

Alikuwa kiongozi wa wajumbe wa vyama tawala katika Seneti kwa kipindi cha 2013 na 2017 na kuwa Naibu Spika wa Seneti kuanzia Agosti 2017 hadi 2020.

Alikuwa wakili wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC).

Prof. Kindiki alipata shahada ya Sheria (LLB) kutoka Chuo Kikuu cha Moi na Diploma ya Mafunzo ya Sheria kutoka Shule ya Sheria ya Kenya.

Pia ana Shahada ya Uzamili katika Sheria ya Kimataifa ya Haki za Kibinadamu na Demokrasia na Shahada ya Uzamivu katika Sheria za Kimataifa, kutoka Chuo Kikuu cha Pretoria, Afrika Kusini.

Awali Prof. Kindiki alikuwa mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Moi.

Pia aliwahi kuwa Mhadhiri Mwandamizi na Mkuu wa Idara ya Sheria ya Umma katika Chuo Kikuu cha Nairobi na baadaye alipanda hadi kuwa Mhadhiri Mshiriki katika Shule ya Sheria katika taasisi hiyo hiyo.

Pia aliwahi kuwa Katibu wa Uwiano wa Kitaifa chini ya Rais Mwai Kibaki.

Msomi huyo mashuhuri katika sheria za Kimataifa na haki za binadamu, amewahi kuwa mshauri wa mashirika ya ndani na kimataifa ikiwa ni pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP.

Kindiki ni mwanachama wa Baraza kuhusu Mfumo wa Umoja wa Mataifa (ACUNS), Chama cha Kimataifa cha Utafiti wa Uhamiaji wa Kulazimishwa (IASFM), Chama cha Wanasheria wa Kenya (LSK) na Tume ya Kimataifa ya Wanasheria, Kenya (ICJ- K).

**BBC**

# Mradi wa uchumi rejeshi kuongeza ubora maji katika Ziwa Tanganyika

**Na Jenifer Gilla**

TAASISI ya Catholic Relief Services (CRS) kwa kushirikiana na Taasisi ya Caritas wameanzisha Mradi wa Uchumi Rejeshi katika maeneo yanayozunguka Ziwa Tanganyika, ili kuongeza ubora wa maji ziwani humo na kuinua uchumi wa wananchi.

Mradi huo unalenga kuongeza uelewa wa namna ya kubadilisha taka kuwa fursa na kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya taka rejeshi kwa makundi mbalimbali kuanzia ngazi ya jamii, wafanyabiashara taasisi binafsi na serikali.

Kupitia ufadhili wa Sh. bilioni 13.2 kutoka Shirika la Umoja wa Ulaya (EU), mradi huo utatekelezwa katika Manispaa ya Kigoma, Uvinza na Kigoma Ujiji nchini na wilaya ya Mpululu, Zambia kwa miaka minne kuanzia Septemba mwaka huu hadi Agosti 2028.

Akiutambulisha mradi huo kwa wadau wa mazingira juzi, jijini Dar es Salaam, Meneja Mradi CRS Tanzania, Robert Muganzi, alisema waliamua kuelekeza mradi huo mkoani Kigoma, ili kuokoa afya za wananchi zilizoko hatarini kutokana na taka kuzagaa Ziwa Tanganyika.

Muganzi alisema mradi huo utaiwezesha serikali kuweka mifumo ya kisheria wa usimamizi wa taka, ili kuwa thabiti ikiwamo kuwabana wazalishaji waweke mifumo mizuri ya kuzikusanya na kuzichakata.

Kupitia mradi huo, wakulima na wafugaji watafundishwa mbinu endelevu za kufanya shughuli zao bila kuathiri maji katika ziwa hilo na kujiepusha na kukata miti, uharibifu wa udongo na uvuvi haramu.

"Tunawafundisha kujiepusha na kilimo ambacho kinasababisha udongo ulioko kando ya ziwa kuingia ziwani na kuharifu chanzo cha maji," alisema. Pia alisema watatoa fedha kwa vikundi vya kinamama vya kuweka na kukopa maarufu kama VICOBA na kuwapatia elimu ya urejeshaji wa taka, ili kuwapa maarifa na mtaji wa kuanzisha biashara hiyo.

Msingi mkuu wa mradi huo ni kujenga uelewa wa pamoja na kufanya ushirikishaji wa wadau katika utekelezaji wa mradi na utazingatia ushirikishaji katika ngazi zote kuanzia vikundi vya kijamii, taasisi binafsi na serikali.

Ofisa Programu wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania, Letizia Beltrame, alisema mradi huo ni muhimu katika maendeleo ya jamii katika nchi hizo zinazozungukwa na Ziwa Tanganyika kwa kuwa itaongoeza umakini katika usimamizi wa maji.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Ecohub, inayojishughulisha na urejeleshaji taka, Sarah Pima aliwapongeza CRS na Caritas kwa kuratibu mradi huo, kwani utasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha maji ya Ziwa Tanganyika, hivyo kulinda afya za watumiaji.

Alipongeza pia EU kwa kufadhili mradi huo akieleza kuwa, uchumi rejeshi bado ni jambo jipya nchini kwa hivyo, utekelezwaji wake utaongeza maarifa na ajira, kuhifadhi mazingira, kukuza uchumi wa mtu mmoja hadi pato la taifa.

"Kubwa nilichokipenda katika mradi huu ni namna utakavyoshirikisha makundi mbalimbali, hili ni la muhimu sana kwa kuwa utekelezwaji wa uchumi rejeshi unahitaji ushirikiano katika ngazi zote kama jamii, sekta binafsi, wafanya uamuzi, wasomi na asasi za kiraia," alisema Pima.



Bajaji zikiwa zimeegeshwa kusubiri abiria pembeni ya maji machafu yaliyotuama eneo la Mtaa wa Kisutu, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii na kusababisha kero na usumbufu kwa abiria wanaotumia usafiri huo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tanzania yapokea bilioni 68/- za barabara za mzunguko Dodoma

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imepokea msaada wa Yeni za Japan bilioni 4.07 (Sh. bilioni 68.5) kwa ajili ya kugharamia mradi wa ujenzi wa barabara za mzunguko za ndani jijini Dodoma.

Akizungumza mkoani Dar es Salaam juzi baada ya utiaji saini wa mkataba huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dk. Natu Mwamba, alisema utekelezaji wa mradi huo utapunguza msongamano wa magari na kuboresha mazingira ya Jiji la Dodoma.

Alisema mradi huo utahusisha utanuzi wa barabara kutoka njia mbili hadi nne kuanzia mzunguko wa Barabara ya Bahi, Image hadi Makulu.

Alisema mradi huo unaendana na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wenye maudhui ya kufikia ushindani na viwanda kwa ajili ya maendeleo ya watu ambao unalenga kuongeza ufanisi na uzalishaji kwa kutumia rasilimali zilizoko.

Alisema mpango wa sasa wa miaka mitano ni sehemu ya kufikia Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025 na ni nguzo muhimu katika maandalizi ya Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2050.

Naye Balozi wa Japan nchini Tanzania, Yasushi Misawa, alisema mradi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko ya ndani jijini Dodoma iliidhinishwa na Baraza la Mawaziri la Japan Agosti 2022.

Alisema mradi huo utawezesha ujenzi wa kilomita 3.1 za barabara mpya na kupanua kilomita 3.4 za barabara zilizoko ndani ya Jiji hilo.

Aidha, alisema kukamilika kwa mradi huo utaendeleza mtandao wa barabara wa korido ya kati inayopita katikati ya Jiji la Dodoma.

Balozi Misawa alisema katika mkutano wa TICAD 7 uliofanyika mwaka 2019 Japan ilisisitiza umuhimu wa kuimarisha uhusiano kati yake na Afrika kupitia bahari ya Indo-Pasific na kuendeleza miundombinu bora inayokuza uunganishaji wa maabara. Alisema: "Nilianza kazi yangu hapa Tanzania Juni 2022 na miezi miwili baadaye Baraza la Mawaziri huko Japan lilifanya uamuzi wa kuunga mkono mradi huu".

Naye Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Dk. Charles Msonde, alisema msaada wa fedha hizo umekuwa wakati mwafaka wakati serikali ikiwa katika mkakati wa upanuzi na ujenzi wa miundombinu ya barabara nchini.

# Wahitimu SUA waaswa kuonesha ufanisi kazini

**Na Christina Haule, MOROGORO**

WAHITIMU 3,061 kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wameagizwa kuwa mabalozi wazuri na kutimiza imani iliyoko kwa jamii na kuonesha ufanisi wanapofanya kazi zao.

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, Jaji Mkuu Mstaafu Mohamed Chande Othman, alisema hayo jana mjini hapa katika mahafali ya 44 ya chuo hicho yaliyohudhurishwa na Mkuu wa Chuo hicho, Jaji Joseph Warioba.

Alisema jamii ya Watanzania inategemea kutoka kwao kuona ufanisi katika kazi watakazofanya.

Jaji Othman alisema baraza linaendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuboresha mafunzo kwa vitendo na kuongeza ujuzi kwa wahitimu.

Aliihimiza menejimenti ya chuo hicho kutilia mkazi mafunzo kwa vitendo, kuboresha mashamba darasa, karakana za uhandisi, maabara na misitu ya mafunzo, ili kutoa fursa kwa wanafunzi na wadau wengine wa kilimo, kujifunza kwa vitendo na kuongeza maarifa, ujuzi na umahili.

Makamu wa Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Raphael Chibunda, alisema wahitimu hao ni kutoka katika ngazi za Shahada, Stashahada na Astashahada ambapo idadi ya wanawake imeendelea kuongezeka na kufikia 1,411 sawa na asilimia 46 ya wahitimu, huku wanaume wakiwa 1,650 sawa na asilimia 54.

Prof. Chibunda alisema, SUA haina budi kujipongeza kwa mafanikio yanayoonekana kila mwaka kwa kuongeza idadi ya nguvu kazi yenye taaluma, ujuzi na weledi ambayo ni chachu ya kuongeza maendeleo katika nchi.

Baadhi ya wahitimu akiwamo, Ismaili Mtulia, aliyehitimu Shahada ya Lishe, alisema watakwenda kutoa elimu kwa jamii ili kuhakikisha suala la udumavu kwa watoto linalosababishwa na ukosefu wa lishe linapungua au kwisha kabisa nchini.

Alisema suala la ukosefu wa lishe limetambulika katika mikoa mbalimbali ukiwamo Mkoa wa Iringa ambapo kupitia elimu waliyoipata, wanaamini jamii itabadilika kwa kutumia kitaalamu mazao wanayolima katika kuboresha lishe za familia zao.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile.
Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.

# Damu ya Mariamu-35

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Habari zikasema kuwa pesa ile sasa ikahamia kwa askari wasio waaminifu ambao kwa kushirikiana na mtoa rushwa, Materu, waliamua kumsaka muuaji feki ili kumbambikia mzigo huo.

Mtu waliomuona ni rahisi kwao na kila mmoja ataamini ni mpenzi wake Kamal, ndipo kwa kushirikiana na baadhi wa waandishi wasio waaminifu, walitengeneza mazingira ya kijana huyo kuonekana muuaji, na hata kuanza kusakwa na polisi.

Wakasema kijana huyo kwa sasa hajulikani alipo kwani anasakwa kwa tuhuma hizo na Jeshi la Polisi, pamoja na genge la Materu kwa ajili ya kummaliza ili kupoteza ushahidi.

Habari hizi zilipotoka nchi ilisisimka. Kila mmoja alirudisha picha nyuma juu ya mauaji ya mrembo Mariam ambayo yalileta tafrani kiasi cha uchunguzi kufanywa mara mbili, mpaka pale kila mmoja alipoamini mpenzi wake alimuua kwa sababu ya kimapenzi.

Leo waandishi wameingia chimbo na kuibuka na uchunguzi kuwa tajiri Materu, ambaye kwa sasa anawania ubunge kwenye moja ya majimbo ya Kilimanjaro ndiyo mhusika mkuu.


Hali ilianza kubadilika, wananchi mitaani walilitaka jeshi la polisi kujitokeza na kuwaambia ukweli wa jambo hili na kama si kweli basi serikali ivichukulie hatua za kisheria magazeti na televisheni.

Kwa upande wake Materu aliita waandishi wa habari na kukanusha kila kitu alichotuhumiwa nacho. Akasema hayo yote yanafanywa na watu ambao anawania nao nafasi ya ubunge Kilimanjaro. Akaahidi kuwafungulia mashtaka wote waliohusika kwani wanawafahamu.

"Hii ni kutaka kunichafua, kisa wanataka ubunge, wanajua kabisa mimi ni kikwazo kwao, kama mimi nikikatwa, wao ndiyo wanaweza kuupata. Nasema nitalinda heshima yangu kwa gharama yoyote ile na nina mpango wa kuwafungulia kesi ya wote walioungana kushunishusha hadhi, ikiwemo vyombo vya habari," alisema Boniface Materu.

Mitaani hali ilikuwa mbaya, kwenye mitandao ya kijamii ndiyo kabisa. Wananchi waligeuka. Walianza kuamini kuwa Kamal hakumuua mpenzi wake.

Walianza kuyaamini yote ambayo yaliandikwa kwenye magazeti. Huko kwenye mitandao ya kijamii zilianza kutolewa sauti na picha fupi za video zilizoonyesha Materu na wenzake wako kwenye kikao cha kupanga mikakati ya kumuua Mariamu, kuua ushahidi wa kifo chake kwa kuwahonga madaktari kupindisha uchunguzi, na hata kumsingizia Kamal kesi.




**Alisema pamoja na yeye mwenyewe kuwa jasiri, lakini askari polisi mmoja mwaminifu, mzalendo, alimsaidia kwa kiasi kikubwa kwa hali na mali, ikiwemo kutoa muda wake na pesa kwa ajili ya kuusaka ukweli na kukusanya ushahidi.**

Shinikizo kubwa lilisababisha Jeshi la Polisi kutoa tamko rasmi ambalo lilitolewa na Mkuu wa Polisi Kanda.

"Baada ya siku mbili tatu za haya yanayosemwa, ikiwemo kuandikwa na magazeti na kutangazwa na baadhi ya televisheni, Jeshi la Polisi limeamua kuanza upya mchakato na uchunguzi wa kifo cha Mariamu.

Tumeamua hivyo kwa manufaa ya wananchi na kuleta haki na utulivu kwa jamii. Kwa maana hiyo tunafuta kauli ya kuwa Kamal ni mtuhumiwa wa kesi hiyo. Kwa sasa hakuna mtuhumiwa mpaka pale polisi tutakapojidhihirisha.

Hivi karibuni tutatangaza jopo la maaskari ambao watafanya uchunguzi wa jambo hili kabla ya kubaini ni nini kimetokea. Kama mtuhumiwa akionekana amefanya basi tutamtangaza tena, lakini kwa sasa kama yupo hai na amejificha sehemu anaweza kutoka na yeye anaweza kuwa sehemu ya ushahidi na yoyote yule ambaye anaufahamu.

Wananchi lazima wajue kuwa ushahidi wetu wa awali unajikita zaidi kwa huu ambao umeanza kutolewa kwenye magazeti na televisheni kama una ukweli ndani yake na sisi tutakwenda mbele zaidi.," alisema.

Tangazo hilo liliwafurahisha wananchi wengi ambao walishaanza kuamini kuwa kifo cha mrembo Mariamu ulikuwa ni mpango uliofanywa na mtu na wala hakuuawa na mpenzi wake Kamal, hivyo alilitaka Jeshi la Polisi kumtoa kwenye tuhuma.

****************************************

Tamko hilo lilimfanya Kamal arejee uraiani. Kurejea kwake kulimfanya kuwa maarufu kwani kila mmoja sasa alitaka kumfahamu ni nani, kwa nini alituhumiwa, alikuwa amejificha wapi, wengine wakienda mbali zaidi kuona kuwa alibarikiwa na msichana mrembo sana ambaye hata wakubwa walimtaka, lakini aliwakataa kwa sababu ya mapenzi makubwa aliyokuwa nayo ambayo yalimsababishia umauti.

Katika mahojiano, waandishi walitaka kujua alitumia njia gani kukusanya ushahidi mgumu kama ule ambao umesababisha kujulikana kama Materu amefanya hivyo.

Alisema pamoja na yeye mwenyewe kuwa jasiri, lakini askari polisi mmoja mwaminifu, mzalendo, alimsaidia kwa kiasi kikubwa kwa hali na mali, ikiwemo kutoa muda wake na pesa kwa ajili ya kuusaka ukweli na kukusanya ushahidi.

Njia iliyotumiwa iliwashangaza na kuwafurahisha mabosi wa polisi, wakivutiwa na ujasiri na mbinu zake, lakini hapo hapo wakiambiwa yupo kijana mmoja wa jeshi hilo ndiye alikuwa kinara ya kusaka ushahidi huo.

Pamoja na mabosi wa polisi kutaka amtaje, alikataa na kusema angefanya hivyo wangeweza kumpa adhabu kwani alikuwa anafanya kazi bila kuambiwa na mabosi wake.

Hata hivyo jeshi la polisi lilimhakikishia kuwa hawatofanya hivyo, badala yake watamwingiza kwenye mmoja wa watu ambao watachunguza rasmi tukio hilo, na kwa sababu yeye alishafanya hivyo mwanzo atarahisisha zaidi upelelezi.

Ndipo Kamal, alipomtaja afande Willy kuwa ndiye kwa kiasi kikubwa aliyeratibu mkakati mkubwa ya kufanya uchunguzi suala hilo ili kujua ni nani aliyehusika na mauaji na Mariamu, baada ya kugundua kuwa mpenzi wake si aliyefanya hivyo.

Mabosi alishangazwa sana, kwani afande Willy ni mmoja wa maafande vijana, wapole, wanyenyekevu, ambapo hawakudhania kuwa angeweza kuwa na mbinu na kipelelezi za hali ya juu kama zile.

Katika kikao chao walikubaliana kuwa afande huyo anaweza kuwa msaada mkubwa na nchi siku zijazo. Hawakumwambia chochote, bali kumtangaza kuwemo kwenye kundi la kufanya uchunguzi sakata lile na yeye aliwekwa kuwa wa pili baada ya afande mmoja wa juu.

Haukuwa uchunguzi mkubwa, mkali, wa kuvutia na wenye misukosuko kama ule wa kina Kamal na afande Willy.

Ni kwa sababu walikuwa wanarudia tu mle mle. Walikuwa wanapata kila kitu kwa urahisi, tofauti na ule wa mwanzo ambao ulibidi utumiwe mbinu za hali ya juu bila kujulikana.

Wiki moja tu, tayari upelelezi ulikamilika na ushahidi ulipelekwa. Haikutofautiana na ule ulioandikwa gazetini na kwenye televisheni. haukuwa tofauti na ule alioutia Kamal ambao ndiyo huo huo aliwapa waandishi.

Kila kitu kilikuwa wazi. Jeshi la Polisi liliamuru Materu akamatwe, ili akafunguliwe mashtaka ya mauaji, yeye na wenzake wanane ambao walishiriki kwa njia moja ama nyingine, wakiwemo waliomuua Mariamu kwa mkono wao.

Haikuwa rahisi kumkamata mtu tajiri kama Materu. Ilibaki kidogo tu afanikiwe kutoroka nchini. Alikamatiwa Namanga akiwa anataka kuvuka mpaka kuingia nchini Kenya.

Akaridishwa Dar es Salaam na kupelekwa rumande akisubiri kesi yake. Wakati huo Kamal na rafiki yake afande Willy walikuwa wamekaa sebuleni na macho yao walimuona Materu kwenye televisheni akiwa amefungwa pingu akirejeshwa Dar. Wakaangaliana, wakatabasamu. Pamoja na kuwa huru na kufanikiwa kurudi nyumbani kwake, bado Kamal alipendelea kuishi kwa rafiki yake huyo kwani walianza kushibana na kuwa kama rafiki wa damu.

*Itaendelea Jumamosi*

# TANZANIA, MOROCCO USO KWA USO FAINALI UFUKWENI

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Ufukweni inatarajia kushuka uwanjani kukutana na Morocco katika mechi ya Kundi A ya Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (BSAFCON 2024), itakayochezwa leo nchini Misri.

Mechi ya ufunguzi ya fainali hizo itawakutanisha wenyeji Misri dhidi ya Ghana ambazo pia ziko Kundi A.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Jaruph Juma, alisema kikosi chake kiliwasili salama nchini humo na wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya mchezo huo wa kwanza.

Juma alisema wachezaji wote wako katika hali njema na wanaahidi watapambana kuhakikisha wanaanza vizuri fainali hizo.

„Tulifika salama hapa Misri kwenye mji wa Hurghada, sehemu ambayo imepangwa kufanyika fainali za Afrika za soka la ufukweni mwaka huu, tunashukuru Mungu hali ya afya ya wachezaji ni nzuri na wana ari ya kupambana.

Mchezo wetu wa kwanza tutaucheza Jumamosi dhidi ya Morocco, ni muhimu kushinda ili kutupa ramani ya kule tunakoelekea, na niwaambie Watanzania kuwa tumejiandaa vizuri sana," alisema Juma.

Kocha huyo alisema mchezo huo hautakuwa mwepesi kwa sababu anaifahamu vizuri Morocco na kila upande unatarajia kufanya vyema ili kufikia malengo ya kukata tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia.

„Niseme utakuwa mchezo mgumu kwa sababu Morocco wamejipanga vizuri kutaka kufuzu kwenda kucheza Kombe la Dunia, lakini nina uhakika sisi tutakuwa kikwazo kwao na kwa yoyote tutakayekutana naye ili kutimiza malengo yetu pia," aliongeza kocha huyo.

Kundi B katika fainali hizo linaundwa na Senegal, Msumbiji, Malawi na Mauritania.

Ratiba inaonyesha Tanzania itarejea tena uwanjani keshokutwa kucheza dhidi ya wenyeji Misri na Oktoba 22, mwaka huu itamaliza mechi zake za hatua inayofuata kuikabili Ghana.



Straika wa Stars Point FC, Jackson Labigambo (kushoto), akiwania mpira dhidi ya Edson Steven wa JMK Park katika mechi ya kirafiki iliyofanyika kwenye Uwanja wa Kidongo Chekundu Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Geita Gold, Sports hapatoshi

**Na Somoe Ng'itu**

GEITA Gold inatarajia kuikaribisha African Sports kutoka Tanga katika mechi ya Ligi ya Championship itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu iliyoko mkoani Geita.

Nahodha wa timu hiyo, Yusuph Mhilu, aliliambia gazeti hili wamejiandaa vyema kuvuna pointi tatu muhimu za mchezo huo kwa sababu wanataka kurejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mhilu alisema wamejipanga kumaliza ‚kazi mapema' kwa kuvuna pointi nyingi katika mechi zote za mzunguko wa kwanza.

„Vita ya kupanda Ligi Kuu ni kubwa, ili tufikie malengo ni lazima tushinde, tuko tayari kupambana kwa dakika zote," Mhilu alisema.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo ni kati ya Mbeya City dhidi ya TMA ya mkoani Kilimanjaro.

Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa Maafande wa Polisi Tanzania kuwavaa Mtibwa Sugar kutoka Turiani mkoani, Morogoro huku Bigman FC inayofundishwa na Kocha Mkuu, Uhuru Selemani ikiwafuata Stand United ya Shinyanga.

## Kocha JKU aanika siri inayowafelisha

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa JKU, Salum Ali amesema aina ya makosa yanayojirudia kwa wachezaji wake yanasababisha timu hiyo kufanya vibaya katika michezo ya Ligi Kuu Zanzibar inayoendelea.

JKU imejikuta katika wakati mgumu baada ya kushindwa kupata ushindi katika michezo minne mfululizo waliyocheza hivi karibuni.

Maafande hao wa JKU SC juzi walijikuta wakilazimishwa suluhu dhidi ya New City FC mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa nje wa New Amaan Complex ‚Annex B'.

Mchezo huo uliohudhuriwa na mashabiki wengi uwanjani huku kipindi cha kwanza timu ya JKU SC ikifanikiwa kuwadhibiti wapinzani wao na kutawala mchezo.

Akizungumza na gazeti hili, Ali, alisema licha ya mchezo huo kuwa mgumu, bado suala la umakini linawasumbua zaidi washambuliaji wake.

Kocha huyo alisema licha ya kufanikiwa kuutawala mchezo na kudhibiti mashambulizi kwa kiasi kikubwa, lakini wanashindwa kupata mabao hata katika nafasi za wazi wanazotengeneza.

Aliongeza safu yake ya ushambuliaji bado haina umakini mzuri pamoja na kufanya maamuzi ya haraka katika kutumia nafasi wanazozitengeneza.

"Hakuna kosa jipya ambalo limeongezeka, makosa ni yale yale ya umakini, pia wanashindwa kufanya uamuzi wa haraka tunapokuwa jirani na lango la wapinzani wetu," Ali aliongeza.

Hata hivyo alisema ataendelea kufanyia kazi makosa hayo ili kuona timu yake inaimarika na kuwa na hamasa ya matokeo kama ilivyokuwa hapo awali.

Kwa matokea hayo, JKU SC imeendelea kubakia katika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar yenye timu 16 baada ya kufikisha pointi 11 wakati New City FC nayo ikibakia katika nafasi ya 14 na pointi zake mbili.

Bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar hupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL YAMTAKA SALIBA

ARSENAL wana imani kuwa mlinzi wa Ufaransa, William Saliba, mwenye umri wa miaka 23, atasalia kwenye Uwanja wa Emirates licha ya Real Madrid kumtaka. ***(Express)***

### CALVERT-LEWIN KUONDOKA

KLABU ya Juventus inaweza kumnunua mshambuliaji wa Everton, Dominic Calvert-Lewin, mwenye umri wa miaka 27, ambaye mkataba wake utamalizika msimu wa joto. (***Corriere dello Sporti***)

### HOENESS ALIIKATAA UNITED

MANCHESTER United walimtafuta Kocha Mkuu wa Stuttgart, Sebastian Hoeness, mwenye umri wa miaka 42, ili kuchukua nafasi ya Erik ten Hag msimu uliopita lakini kocha huyo aliwakatalia. ***(Bild)***

### PENDERS KUTUA CHELSEA

CHELSEA imejiweka kifua mbele msimu uliopita walipoishinda Bayern Munich katika kuinasa saini ya mlinda mlango wa Genk, Mike Penders, mwenye umri wa miaka 19, na raia wa Ubelgiji, ambaye atahamia Stamford Bridge Julai mwakani. (***Fabrizio Romano***)

### OYEDEJI ATAKIWA UJERUMANI

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Nathan Butler-Oyedeji, mwenye umri wa miaka 21, anawindwa na Borussia Monchengladbach ya Ujerumani. ***(Football Insider)***

### FRIEDRICH NJIA MOJA

MLINZI wa kati wa Ujerumani, Marvin Friedrich, mwenye umri wa miaka 28, anaweza kuondoka Borussia Monchengladbach ifikapo Januari. ***(Sky Sport Germany)***

### ARSENAL, SPURS VITANI

ARSENAL imeungana na Tottenham Hotspur katika kinyang'anyiro cha kuwania huduma ya kiungo mshambuliaji wa Timu ya Taifa Ukraine, Georgi Sudakov, mwenye umri wa miaka 22 kutoka Shakhtar Donetsk. ***(Caught Offside***)

### SANE AGOMBEWA ENGLAND

BARCELONA, Arsenal na Newcastle United zote zimeonyesha nia ya kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Leroy Sane, mwenye umri wa miaka 28 kutoka Bayern Munich. ***(Ekrem Konur)***

### DIBLING SOKONI RASMI

KLABU ya Southampton imesema inamatumaini ya kumshawishi kiungo wa kati wa England, Tyler Dibling, mwenye umri wa miaka 18, kusaini mkataba mpya huku Manchester United wakionyesha nia ya kutaka kumnunua yosso huyo. ***(GiveMeSport)***

### SUNDERLAND YAMTAKA CONNOLLY

KLABU ya Sunderland inajipanga kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Brighton na Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Ireland, Aaron Connolly, mwenye umri wa miaka 24, kutoka Hull City. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BARCA ILIKATAA DAU KUBWA KWA YAMAL

●●● Rais Laporta asema aliamini nyota huyo atakuwa...

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, amesema klabu hiyo ilikataa ofa yenye thamani ya dola milioni 270 ili kumuuza mshambuliaji, Lamine Yamal, katika majira ya joto.

Laporta hakuweka wazi ni nani alitaka kumsajili, Yamal, lakini ripoti mbalimbali zimeeleza Paris Saint-Germain ilimtaka kijana huyo kuchukua nafasi ya Kylian Mbappé, ambaye alijiunga na Real Madrid mapema mwaka huu.

Laporta alifichua hayo alipokuwa akitetea uamuzi wa Barca kuwaruhusu wachezaji fulani kuondoka, akikana matatizo ya kifedha ya klabu hiyo yalilazimisha mkono wao wa kwa heri katika hali fulani.

"Kuna wale ambao wanadhani tuna wachezaji waliohamishwa ili kusawazisha akaunti," alisema Laporta katika mahojiano na kituo cha televisheni cha ndani cha Barca.

"Lakini sivyo ilivyo, wachezaji waliondoka wameondoka kwa sababu za kimichezo.

"Ousmane Dembélé, Marc Guiu hawakuwa na mambo mazuri.

"Tunajua tunachofanya katika soko la uhamisho. Tunataka wale ambao ni bora zaidi na wanaotaka kuwa hapa wabaki, na tumeonyesha hilo.

"Klabu (hajataja jina), ilikuja kwangu kumsajili Lamine Yamal kwa dola milioni 250 na nikasema hapana."

Tangu acheze kwa mara ya kwanza katika timu yake akiwa na umri wa miaka 15 mnamo 2023, Yamal amekuwa mchezaji wa muhimu kwa klabu na nchi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17 tayari ameshacheza zaidi ya mechi 60 akiwa na Barca na alichukua jukumu muhimu Hispania ilipotwaa ubingwa wa Ulaya.

Katika mahojiano na ESPN wiki hii, Cesc Fabregas, alimtaja Yamal ndiye kipaji kikubwa zaidi katika soka la dunia.



## Liverpool wanajua Alexander-Arnold ataondoka

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL imeripotiwa inajua itampoteza Trent Alexander-Arnold hapo mwakani, ambaye ameibuka kama shabaha kuu ya Real Madrid.

Mhitimu huyo wa akademi ya klabu hiyo alikuwa ndani ya umbali wa kutembea wa uwanja wa zamani wa mazoezi wa Liverpool, akipanda juu ya uzio ili kupata picha ya wachezaji anaowapenda.

Baada ya kujiimarisha kama mmoja wa mabeki wa kulia wanaoongoza duniani wa kati, mkataba wa sasa wa Alexander-Arnold utaisha ifikapo Juni mwaka, 2025.

Kwa mujibu wa ripoti ya jarida la Hispania la Marca, kumekuwa hakuna mawasiliano ya moja kwa moja kati ya klabu hizo, lakini Madrid inasemekana inajua Alexander-Arnold hataongeza mkataba wake na Liverpool.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England amekuwa na utata wakati akizungumzia mada ya mkataba wake unaoisha.

Marca hata ilipendekeza Madrid inaweza kujaribiwa katika harakati za msimu wa baridi wa Alexander-Arnold kutokana na kuongezeka kwa majeraha katika safu ya nyuma ya klabu.

Chaguo la kwanza la beki wa kulia, Dani Carvajal atakosa msimu uliosalia baada ya kuumia na kumwacha winga wa zamani Lucas Vazquez mwenye umri wa miaka 33 kama beki pekee mkuu wa kulia.

Iwapo Alexander-Arnold atakuwa mchezaji wa kwanza kusajiliwa katika majira ya baridi ya Madrid tangu COVID-19, klabu hiyo ya Ligi Kuu England itadai kiasi kikubwa cha fedha.

The Athletic inasisitiza mbinu ya kumnunua Alexander-Arnold itawezekana tu ikiwa atamaliza mkataba wake na Liverpool, lakini kuthibitisha Madrid wamemfanya beki huyo wa kulia kama kipaumbele chao.

# Mourinho ajiandaa kumsajili Ansu Fati

**ANKARA, Uturuki**

KOCHA wa Fenerbahce, Jose Mourinho anaripotiwa ameonyesha nia ya kumsajili kinda aliyefifia wa Barcelona, Ansu Fati katika dirisha la Januari.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania aling'ara Ulaya akiwa kijana mdogo na kuweka rundo la rekodi zinazohusiana na umri kwa Barcelona na Timu ya Taifa ya Hispania.

Fati anasalia kuwa mfungaji mabao mwenye umri mdogo zaidi katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, akifumania nyavu kwa wababe hao wa Katalunya dhidi ya Inter mwaka, 2019 ikiwa ni takriban mwezi mmoja tu tangu kutimiza miaka 17.

Mourinho hana sifa kubwa ya kukuza vijana lakini anataka sana kumleta Fati Fenerbahce, kulingana na chapisho la gazeti la AS.

Winga huyo wa Barcelona atafikisha umri wa miaka 22 mwezi huu mwishoni na amekuwa na majeraha mengi tangu alipoumia uti wa mgongo hapo Novemba mwaka, 2020.

Kocha huyo raia wa Ureno anayezungumza waziwazi alitaka kupata dili la kumnunua Fati wakati wa dirisha lake la kwanza la uhamisho, na anasisitiza makubaliano ya mkopo yatafutwa Januari.

Fati alitumia msimu uliopita kwa mkopo akiitumikia Brighton.

Baada ya mwanzo mzuri kuleta mabao mawili katika mechi zake tano za kwanza za Ligi Kuu England, fowadi huyo mahiri alipoteza nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza kutokana na jeraha la mguu.

Hata baada ya kurejea katika utimamu wa mwili, Fati hakufanikiwa kumshawishi, Roberto De Zerbi, kumnunua.

Dakika zimekuwa ngumu kufikia sasa baada ya kurejea Barcelona. Hansi Flick bado hawajamwanzisha Fati msimu huu.

## MAINOO KUIGHARIMU MAN UNITED

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United imethibitisha inatarajia kumkosa kiungo wake, Kobbie Mainoo, katika michezo michache ijayo kutokana na kusumbuliwa na majeraha.

Mainoo aliondolewa dakika tano kabla ya mchezo kumalizika United ilitoka suluhu dhidi ya Aston Villa, mechi iliyochezwa kabla ya mapumziko ya kimataifa.

Baada ya hapo Mainoo alijiondoa kwenye kikosi cha England kwa mechi dhidi ya Ugiriki na Finland kama „tahadhari", lakini tatizo lake sasa limefichuliwa ni kubwa zaidi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 hapo awali pia alilazimika kutolewa nje kutokana na jeraha katika kipindi cha kwanza cha kichapo cha 3-0 kutoka kwa Tottenham Hotspur mwezi uliopita, akiwa nje ya pambano lililofuata walipocheza dhidi ya Porto.

Kabla ya kumenyana na Brentford katika Ligi Kuu England leo United wamethibitisha Mainoo atakuwa nje ya uwanja kwa „wiki chache" kutokana na jeraha la misuli.

Mainoo ameanza kila mechi ya Ligi Kuu kwa United hadi sasa msimu huu.

Kati ya sasa na mapumziko ya kimataifa ya Novemba katika wiki nne, timu ya Erik ten Hag ina michezo saba katika mashindano matatu.

Kuanzia na Brentford wikendi hii, tahadhari inageukia kwa Ligi ya Europa kwa safari ndefu ya kwenda na kurudi Istanbul kumenyana na Fenerbahce halafu itakutana na West Ham United kwenye Uwanja wa London na itafuatiwa na mechi dhidi ya Leicester City katika Kombe la Carabao siku tatu baadaye.

HABARI MICHEZO

# MINZIRO ATAMBA KUWAPA FURAHA PAMBA JIJI KESHO

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu mpya wa Pamba Jiji FC, Fred Minziro, amesema anaamini ataipa ushindi wa kwanza timu hiyo itakapoikaribisha Kagera Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Minziro ametua Pamba Jiji akirithi mikoba iliyoachwa na Goran Kopinovic, baada ya Mserbia huyo kushindwa kuipa matokeo chanya.

Kagera Sugar pia itashuka dimbani katika mchezo huo ikiwa na kocha mpya, Melos Medo, ambaye amechukua nafasi ya Paul Nkata, aliyetimuliwa hivi karibuni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Minziro alisema amewaandaa wachezaji wake kucheza soka la utulivu na kuondoa wasiwasi katika mechi hiyo.

Minziro alisema anawaheshimu Kagera Sugar na anaamini mechi hiyo itakuwa na ushindani kwa sababu kila upande utaingia kurekebisha makosa ya michezo iliyotangulia.

"Wachezaji wangu wako katika hali nzuri, ninaamini maandalizi tuliyofanya yatatupa matokeo mazuri, ninaijua vizuri Ligi Kuu na Kagera Sugar ninaifahamu pia, tutarajie mechi yenye ushindani," Minziro alisema.

Naye Mtendaji Mkuu wa Kagera Sugar, Thabit Kandoro, aliliambia gazeti hili kikosi chao kimefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo huo.

Kandoro alisema wamejiandaa kukutana na ushindani kwa sababu wapinzani wao pia hawajapata matokeo bora katika michezo iliyotangulia.

"Tumerekebisha mapungufu na makosa tuliyoyabaini, tunaamini tutakuwa na mwanzo mzuri na kocha wetu, tumejipanga kuwaletea furaha mashabiki wetu, tunajua wanapitia wakati gani timu inaposhindwa kuwapa kile walichokitarajia," alisema Kandoro.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea leo kwa Simba kuikaribisha Yanga wakati mechi nyingine itakayochezwa kesho ni kati ya Singida Black Stars dhidi ya Namungo FC.



Wachezaji wa Kagera Sugar wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Pamba Jiji FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza. **PICHA: MTANDAO**

# Tanzania yafuzu AFCON U-20

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), imefuzu kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON U-20) baada ya kuifunga Uganda mabao 2-1 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana.

Ngorongoro Heroes itaungana na mshindi kati ya Kenya au Burundi kuiwakilisha CECAFA katika fainali hizo zitakazochezwa kuanzia Septemba 24 hadi Oktoba 13, mwakani nchini Congo Brazzaville.

Ngorongoro Heroes ililazimika kusubiri hadi dakika za lala salama ndani ya dakika 30 za nyongeza kupata bao hilo la ushindi lililofungwa na Jammy Jammy.

Dakika 90 za kawaida zilimalizika timu hizo kuwa sare ya bao 1-1, katika mechi iliyokuwa na ushindani kwa dakika zote, kila timu ikitumia nguvu kusaka mabao.

Uganda ndio walikuwa wa kwanza kupata bao dakika ya 50 kupitia kwa nahodha wao, Toto Bran aliyefunga kwa kichwa.

Bao la kusawazisha la Ngorongoro Heroes lilifungwa kupitia kiungo Mzanzibari Sabri Kondo.

Nusu Fainali nyingine ya michuano hiyo ya CECAFA ilitarajiwa kufanyika jana usiku kwa kuwakutanisha Kenya dhidi ya Burundi.

## Mechi ya kisasi, heshima

INATOKA UK. 24

mchezo huo kwa umuhimu wa kipekee na wanaona wana deni la kuwalipa mashabiki wao ambao muda wote wamekuwa wakiwaunga mkono.

"Tupo tayari kwa mchezo, tumefanya maandalizi ya kutosha, tutapambana kuhakikisha tunawalipa mashabiki wetu upendo, hamasa yao kwetu kama wachezaji," alisema Zimbwe Jr.

Aliongeza wamesahau yote yaliyotokea katika michezo iliyopita walipokutana na wapinzani wao na sasa wanataka kufungua kurasa mpya.

"Mashabiki waendelee kutusapoti, tutapambana kwa kila namna kuhakikisha tunapata ushindi," alisema beki huyo mkongwe ambaye pia anaichezea Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Rekodi zinaonyesha utakuwa ni mchezo wa 29 kuchezwa tangu Ligi Kuu Tanzania Bara 2010/11, huku timu hizo zikiwa tayari zimeshakutana mara 28 mpaka sasa.

Wageni Yanga wanaongoza kushinda michezo mingi, wakiwa wameifunga Simba mara tisa, Mnyama akifunga mabao saba na sare mara 13, katika mchezo ya ligi tu.

Yanga inaingia uwanjani ikiwa imeshinda michezo yote ya Ligi Kuu msimu uliopita ikianza kwa mabao 5-1, mechi iliyopigwa Novemba 4, mwaka jana, mchezo wa mzunguko wa kwanza, huku ikipata tena ushindi wa magoli 2-1, Aprili 20, mwaka huu.

Rekodi zinaonyesha ushindi mkubwa kwenye michezo ya Ligi Kuu tangu msimu wa 2010/11, ni ule wa mabao 5-1 ilioupata Yanga, na ule ya Mei 6, 2012, Simba ilipowachakaza mabingwa hao watetezi mabao 5-0.

Rekodi ya jumla ya juu zaidi iliwekwa na Simba, Julai 19, mwaka 1977, ilipoifunga Yanga mabao 6-0, ambayo haijafutika hadi leo, huku nyingine ikiwa ya Abdallah Kibadeni kufunga 'hat-trick', haijavunjwa na mchezaji yoyote kabla ya mchezo wa leo.

Sare ya mabao mengi kwa timu hizo kwenye michezo ya Ligi Kuu tangu msimu huo ilikuwa ni ya Oktoba 20, mwaka 2013, zilipotoka sare ya mabao 3-3, Yanga akitangulia kufunga mabao matatu na Simba kurejesha walipoingia kipindi cha pili.

Hata hivyo jumla ya sare yenye mabao mengi ni ile ya mabao 4-4 ambazo timu hizo ziliipata zikicheza kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha Novemba 9, mwaka 1996.

Ni straika wa Simba pekee, Leonel Ateba, ndiyo ataonja joto la dabi hiyo kwa mara ya kwanza ukiacha wachezaji wengine ambao walikutana katika mchezo wa Ngao ya Jamii uliochezwa Agosti 8, mwaka huu, Wekundu wa Msimbazi wakilala kwa bao 1-0, nyota huyo alikuwa hajasajiliwa.

Mwamuzi, Ramadhan Kayoko wa Dar es Salaam anatarajiwa kuchezesha mechi hiyo akisaidiwa na Mohammed Mkono wa Tanga na Kassim Mpanga (Dar es Salaam), huku mwamuzi wa akiba akiwa ni Tatu Malogo wa Tanga.

# Michezo

Jumamosi Oktoba 19, 2024

Nipashe


Barca ilikataa dau kubwa kwa Yamal

UKURASA 21





Gamondi

Fadlu

# MECHI YA KISASI, HESHIMA

## ●●●Gamondi, Fadlu wafunguka muda wa vitendo kuzungumza umefika...

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

HATIMAYE siku imefika, watani wa jadi nchini, Simba wanatarajia kuikaribisha Yanga katika Dabi ya Kariakoo itakayochezwa leo kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mbali na dabi zote kusubiriwa kwa hamu na mashabiki wa pande hizo mbili, mechi ya leo itatizamwa zaidi na Wekundu wa Msimbazi ambao wamefungwa katika dabi tatu mfululizo zilizopita.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema kwake mchezo huo ni kama michezo mingine ingawa amekiri ni mchezo mkubwa na wenye hisia kali.

Gamondi alisema wachezaji wake wapo katika hali nzuri na kila mmoja anatamani kuwa sehemu ya kikosi kitakachopambana kusaka ushindi kwenye mchezo huo wa leo.

"Tumejiandaa vizuri, nafahamu kwa sasa Simba wanakikosi kizuri lakini sisi pia tumejiandaa, tutacheza kama tunavyocheza kwenye michezo yetu mingine," alisema Gamondi.

Alisema amewaandaa wachezaji wake kuongeza utulivu wanapokuwa na mipira lakini pia kutowaruhusu wapinzani kutawala mchezo.

Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, aliliambia gazeti hili wachezaji wote wapo tayari kwa ajili ya mchezo huo muhimu na malengo yao ni kuendelea ubabe.

"Hautakuwa mchezo mwepesi hata kidogo, Simba na Yanga ni mchezo mkubwa na wenye presha, lakini tumejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo huu na naamini tutapata matokeo mazuri," alisema Mwamnyeto.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, alisema wanaiheshimu Yanga lakini wapo tayari kupambana uwanjani na wamefanya maandalizi mazuri ya kuwakabili.

Fadlu alisema faida kubwa waliyonayo wapinzani wao ni kuwa na wachezaji waliokaa pamoja kwa muda mrefu na kujenga uelewano mzuri.

"Lakini hiyo bado sisi sio sababu ya kutuzuia kufanya vizuri kwenye mchezo huu, tumejiandaa vizuri na naamini tutapata matokeo mazuri, mashabiki waje kwa wingi uwanjani, hatutawaangusha," alisema Fadlu.

Mohamed Hussein ‚Zimbwe Jr', nahodha wa Simba, alisema wanafahamu umuhimu wa mchezo huo na matarajio ya mashabiki wao baada ya dakika 90 ni kupata ushindi.

Beki huyo alisema wanauchukulia

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >